Readers

uo cha

nasomo.

NON-CIRCULATING

PL8702
.C45x

Mission Bagamoyo

Digitized by the Internet Archive
in 2011 with funding from
LYRASIS Members and Sloan Foundation

http://www.archive.org/details/chuochamasomo00unse

Chuo cha masomo.

~~Spelling~~ book (reader)

DUQUESNE UNIVERSITY LIBRARY
PITTSBURGH 19, PA

R. C. Mission Bagamoyo.

i *ù* *t* *i*

ti *tu* *it* *ut*

n *m* *n* *m*

PL 8702
C45x
afs. Call.

ni *mi* *nu* *mu*

v *v* *v* *v*

vi *vu* *vi* *vu*

i u t u n t i m
n u m t i u n m
tu ti nu ni mu mi
ti mi nu tu mi ni

---

v w u v n w m t
n v m w t i u n
ni mi vi wi vu wu tu
vu wi mu nu vi wi ti

---

ni-ni mi-mi mi-ti vi-tu
vu-mi vi-vi wi-vu wi-vi
ti-ni vi-ti tu-nu mi-ni
mi-ti vu-mi wi-vu ti-ni

MAR 13 1964

a d o

ai di oi du au

oi od do ao ou

e l b

ei li bi lu bu

ea la ba lo bo

a d o d a u a o

da do di du da du
ta du tu da to di

---

e l b e o l a e

la be lo bi lu ba li
to bo tu lu bi la ta

---

ba-ba ma-ma da-da la-la
du-du na-ni wa-tu vi-tu
bo-ma mi-to mu-me wo-te
ba-bu wa-le li-ni me-no

j y g j y g

jï ya go ju yi

ja yo gu jo gi

p f f p

pa fa pu fu po

fi pi fo pe fe

j y g y j g j y

ja ya ga yi go jo yu

yo ji gi ya gu ja go

---

p f g p f j f p

pa fu po fa pi fo

pu fi pe fu po fe

---

ya-yi	**ja-na**	**pa-na**	**fu-no**
fu-pi	**pi-ga**	**li-pa**	**pe-po**
go-ma	**yu-pi**	**bo-ga**	**wa-pi**
wa-fu	**bi-la**	**vu-ja**	**yo-te**
ji-pu	**da-fu**	**wa-li**	**fu-pa**
bu-yu	**wi-no**	**ya-le**	**ji-bu**

h k ch

ha ki che ko hu cha

chu ku ho chi ka hi

---

s r x

sa ro xu si ru sa

xi so ra xe se re

h k ch k l ch h

ha ki che ku ho cha
hu ko he chi ku chu

---

s r z r s z s r z

so ro za si ru sa zi
ro su ri zo sa ra zu

---

so-ma ho-ma ko-pa cho-ma
ho-fu ki-su che-za fu-pi
zi-ko chu-pa ra-zi re-fu
chu-ra he-ri che-ka sa-fi
gi-za du-ka ku-cha me-za
mo-yo wa-zi wa-ko ga-ri

sh ṅ nj sh ṅ

sha ṅo ṅji ṅo shu

mama nini moto vitu

baba hodi hila jiko

fupi meza chafu gari

mvitu duka shoka sūra

sh ch ṅ nj sh ṅ

sha ṅo nji shu ṅa nja

sho-ka ṅa-ra nji-a ṅo-a

shi-ba nji-wa shu-ka nja-a

Ba-ra	be-ga	bi-bo	bo-ko	bu-zi
Pa--ka	pepo	pi-pa	po-no	pu-a
Da-da	de-ni	di-ni	do-do	du-du
Ta-ta	te-te	ti-ni	to-to	tu-tu
Ga-ri	ge-ni	gi-za	go-go	gu-gu
Ka-li	ke-sho	ki-sa	ko-ko	ku-ku
Cha-li	che-che	chi-ni	cho-yo	che-ka
Za-ko	ze-ze	zi-zi	zo-te	zu-zu

Sa-ga	se-zo	ṣi-si	so-ko	su-ra
Sha-da	she-le	shi-na	sho-ka	shu-ka
La-la	le-le	li-ma	lo-zi	lu-lu
Ra-ha	re-fu	ri-za	ro-ho	ru-vu
Ma-ma	me-no	mi-wa	mo-to	mu-da
Ṅa-ra	ṅo-a	ṅom-be		ṅam-bo
Na-ne	ne-no	ni-ni	no-no	nu-ka
Fa-ru	fe-ka	fi-to	fo-ko	fu-pi

da-mu	ma-we	ta-no	ka-zi	yu-pi
hu-ru	ho-ho	lo-zi	ta-tu	fu-pi
vi-su	bo-ma	ku-cha	shi-ba	ji-no
ha-ri	so-da	ta-ka	bi-chi	ni-pe
wa-zi	homa	lu-lu	ta-ta	pi-ga

meza	neno	nani	sumu	shimo
damu	kisu	hema	bara	robo
vita	choka	sala	zuri	lipa
bivu	fito	jana	gari	pesa
moto	tawi	dobi	yako	siki
zika	wali	vuta	ficha	dawa
kuja	pepo	nawa	hima	buni
zima	fupi	saga	chini	shina
dini	maji	posho	zako	haki

apa	ana	ona	iba	ezi	ipi
uzi	oza	upo	aga	ovu	epa
una	osha	ina	uso	ile	iko
pua	tia	chui	leo	juu	mua
kiu	pia	chuo	vua	mia	cheo
ao	ua	oa	uji	acha	jua

Kisu chake na kisu chako. Kiti cha mama yako na cha baba yake. Lete kiti na lete maji. Nina kiu sana leo, lete maji, nipe maji. Paka yake. Lete maji.

Watu wema; watu wale si wema; watu hawa wema sana. Watu gani hawa? Watu wema, watu hawa; wote wema.

Watu hawa woga sana. Watu wote woga? Wote woga. Watu wema si woga, watu wabaya woga. Watu hawa wabaya? Wote wabaya sana, siwataki.

Baba huyu yake. Taa hii kubwa. Kazi yake. Jua kali leo. Dawa yake kali. Mama yako ni yule. Watu hawa wema.

Dafu lako tamu. Nani huyu? Dada yako. Ewe, fua nazi. Miti ile. Maji haya haba. Papa hapa pema. Nazi kavu zile. Maji mema sana. Pana maji hapa. Nipe kisu. Piga kofi.

Neno moja tu. Jiwe moja dogo. Watu wema wale. Jina lako nani? Damu yake. Nipe maji ya moto. Mali ya watu. Dawa ya watu. Zeze lako. Maji haya ya wapi? Kisa cha bibi. Kiko chako. Lete chayi. Piga chapa. Lete kuku ile.

Maziwa	makasi	nahoza	nukato
karibu	kaburi	labuda	lazima
begani	bomani	vilima	vibaya
dirisha	domoni	funika	furahi
zahabu	zimika	rafiki	risasi
samaki	somesha	poteza	pigano
chukiza	chipuko	karibu	gereza

kupika	jaribu	hesabu	kuwasha	ruhusa
labuda	kidogo	kuzima	majini	samani
maliza	kikapo	makucha	mapera	shuhuli
maziwa	kitabu	mayayi	mikeka	tezama
minazi	kucheza	mimina	jikoni	wakati

---

mba	mbe	mchi	mcho	mda	mdu
mfa	mfo	mgi	mgu	mli	mlo
mna	mni	mpo	mpa	msa	msi
mto	mti	mwa	mwi	mru	mri

---

mbeba	mfano	mdogo	mgeni	mji
mkeka	mlima	mnara	mpaka	mto
mshale	mrima	mpera	mwili	mti
mhogo	msitu	mtoto	mzigo	mtu

---

bwa	bu-a	kwa	ku-a	chwa	chu-i
ja	di-a	twa	ti-a	twe	tu-e
ncha	nchi	nja	nji	nda	ndi

---

ndani	ndugu	kunde	njaa	njia
anza	nzito	nyota	nyuma	anga
banda	bonde	chombo	donda	embe
fimbo	fundo	hiyo	inchi	kichwa
lindo	macho	mwanzo	njaa	omba
panya	rangi	samli	shingo	unga
vunja	zambi	zangu	pango	ovyo

Harfu ndogo

a	b	ch	d	e	f
a	*b*	*ch*	*d*	*e*	*f*
g	h	i	j	nj	k	l
g	*h*	*i*	*j*	*nj*	*k*	*l*
m	n	ṅ	o	p	r
m	*n*	*ṅ*	*o*	*p*	*r*
s	sh	t	u	v	w
s	*sh*	*t*	*u*	*v*	*w*

y	z
y	*z*

Harfu kubwa

A	B	Ch	D	E	F
A	*B*	*Ch*	*D*	*E*	*F*
G	H	I	J	K	L
G	*H*	*I*	*J*	*K*	*L*
M	N	Ṅ	O	P	R
M	*N*	*Ṅ*	*O*	*P*	*R*
S	Sh	T	U	V	W
S	*Sh*	*T*	*U*	*V*	*W*
		Y	Z		
		Y	*Z*		

1 . . . moja
2 . . . mbili
3 . . . tatu
4 . . . nne
5 . . . tanu
6 . . . sita
7 . . . saba
8 . . . nane
9 . . . kenda
10 . . . kumi
11 . . . kumi na moja
12 . . . kumi na mbili
13 . . . kumi na tatu
20 . . . ishrini
21 . . . ishrini na moja
22 . . . ishrini na mbili
30 . . . selasini
40 . . . arbaini
50 . . . hamsini
60 . . . sitini
70 . . . sabuini
80 . . . semanini
90 . . . tisini
100 . . . mia
101 . . . mianamoja
102 . . . mianambili
110 . . . mia na kumi
111 . . . mia na kumi na moja
150 . . . mia na hamsini
166 . . . mia na sitini na sita
200 . . . mia mbili (miteini)
300 . . . mia tatu
333 . . . mia tatu na selasini na tatu
900 . . . tisa mia
1.000 . . . alfu
2.000 . . . alfu mbili (alfeini)
10.000 . . . alfu kumi
100.000 . . . alfu mia (lakki)

VITUO.

Vituo ni alama yênyi kupambanua matengeneo ya maneno.

Vituo vilivyofaa zaidi ni:

1. Mkato (,) ndiyo alama yênyi kupambanua maneno na viungo vya matengeneo;

2. Nukta (.) ndiyo alama ya kufunga maana ya matengeneo ya maneno;

3. Nukta na mkato (;) ndiyo alama yênyi kupambanua viungo vya matengeneo;

4. Nukta mbili (:) ndiyo alama yenyi kufungua maana ya maneno;

5. Nukta ya kuuliza (?) ndiyo alama ya kuuliza;

6. Nukta ya kusangaa (!)

7. Asema (« ») ndiyo alama ya maneno yaliyonenwa na mtu;

8. Alama za kati ( ) ndiyo alama ya kupambanua maneno yaliyokuja kati.

SEHEMU YA KWANZA.

1. KUNA MUNGU

I

Yote yamtaja Mungu! Majani ya porini, maua ya bustani, miti ya mwituni, maji ya baharini, mawe ya vilimani, hatta kidudu kinacholia maguguni, na simba anaonguruma kiwalani, na mawingu yanayopita juu, na nyota zinazoñara uwinguni yote yamtaja Mungu Mwiny'ezi, Mkubwa wetu, Bwana wetu, Baba wetu!

II

Kweli, katika vitu vyote hakuna kitu kiwezacho kuanza peke yake. Tukiona nyumba twasema, nyumba hii ikajengwa na fundi. Basi tukitezama jua, mwezi, nyota, nchi, maji, miti, nyama, watu, vitu vyote vilivyomo ulimwenguni, twaona hakika, kwamba yuko Mungu Mwiny'ezi aliyeumba vitu vyote, ndiye Fundi mkubwa! Nani, asipokuwa Mungu, angaliweza kufanya nchi na uwingu?

III

Basi, nasi tumtaje Mungu vile moyoni mwetu, tumpende, tufuate sharia yake, tumtumikie!

Zamani za kwanza Mungu alikuwa peke yake. Nchi haikuwapo bado, wala mwezi, wala jua, wala nyota, wala upepo, wala kitu chochote.

Basi Mungu akasema: Ulimwengu uwe, ulimwengu ukalipo.

Ulimwengu ni kama nyumba ya Mungu. Nae Mungu akaweka jua kama taa ya mchana; akaweka mwezi na nyota kama taa za usiku.

2. MUNGU MUUMBA VITU VYOTE.

Killa alilotaka Mungu akaliumba: akaumba malaika wasio na mwili; akaumba bin-Adamu, walio na mwili pamoja na akili; akaumba nyama, wasio na akili; akaumba miti isiyo na kusikia; akaumba mawe yasio na kuchipuka, akaumba maji yasio na kikao; akaumba upepo usio na kushikwa.

3. MBUZI WAWILI.

Siku moja, mbuzi
Kênda ulaloni,
Ulaloni mdogo,
Na chini, kuna mto.

Mwingine akaja
Nae akalia:
« Simile! nipite!
— Simile na weye!
Mimi mwinyi njia,»
Mbuzi akasema.
Basi ulaloni,
Wote wakaidi,
Washindana,
Wapigana
Saa nzima.
Haya! haya!
Kêsha na wawili
Wakânguka mtoni.

4. MTU BIN-ADAMU.

Mungu amemwumba bin-Adamu, akampa kwenda kiwimawima kichwa juu, macho yake yaelekee uwingu.

Akampa mikono ya kushikia; na miguu ya kwendea; na macho ya kuangalia; na masikio ya kusikia; na pua ya kutolea pumzi, na kuonea arufu; na ulimi wa kunenea maneno; hasa, akampa roho yenyi akili ya kumjulia na kumpendea ye Mwenyewe, kana Muumba na Baba yake.

5. MAMBO YA KUTENDA KILLA SIKU.

Ukitaka kuwa mtu mwema, kumbuka, sherti ukae na moyo safi, usio na zambi ya mauti mpaka kufa.

I
UNAPOAMKA

1. Kwanza fanya ishara ya Msalaba, sema:
„Kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina. — Mungu wangu, nakupa moyo!
2. Ondoka kitandani marra moja, wala usifanye uvivu.
3. Vaa nguo upesi, vizuri, nawa uso na mikono.
4. Kesha, twaa maji ya mbaraka, piga magoti, sali Sala ya Usubuhi.

II
UNAPOFANYA KAZI

1. Ukitaka baraka katika kazi yako, sema kwanza ya kufanya kitu:
„Ewe! Mungu wangu, unibarikie mimi na kazi yangu!“
2. Kesha kazi sema pia:
„Ewe! Mungu wangu, unibarikie mimi na kazi yangu!“

III
UNAPOPUMZIKA

1. Kupumzika, kuzungumuza, kucheza, kutembea, hayo yote si vibaya: kumbuka tu usitende kitu

chenyi kumchukiza Mungu wala kitu cha kumzuru jirani wako, wala kitu cha kuuchafua moyo wako.

2. Hatta wakati huo wa kuzungumuza na kutembea, ukipata nafasi ya kumseidia mtu, au ya kumpa shauri ngema, au ya kumrudisha mwinyi amekosa, au ya kutenda neno lolote jema, usiache: faida yako kesho kwa Mungu.

IV

UNAPOONA MASHAKA, VISHAUSHI.

1. Ukiona mashaka, ugonjwa, uchungu wo wote, vumilia, mshukuru Mungu, sema:

„Ewe! Mungu wangu, ndiwe umetaka; utakalo lifanyike!“

2. Ukiingiwa na vishaushi, mawazo maovu, tamaa mbaya, hayo yote uyatupie mbali upesi, upesi; ukitaka kucheza na mitego ya shetani, utanasa, utalia. Basi kamfukuze marra; sema:

„Yesu na Maryamu njooni kuniopoa: mimi mtoto wenu!“

3. Hatta, ukikosa, mwelekee Mungu; sema:

„Mungu wangu! Baba wangu! nimekosa, natubu, sitaki kufanya marra ya pili.“

V

UNAPOKULA

1. Usile kwa ulafi, hasa usinywe kitu chenyi

kulevya; ulevi wamtoa akili bin-Adamu, wamfanya kama nyama.

2. Kwanza ya kula sema:

„Utubarikie, Mungu, sisi pamoja na chakula chetu, mapaji yako! Kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho-Mtakatifu. Amina.“

3. Kesha kula sema:

„Tunakushukuru weye, Mungu, kwa mapaji yako ya leo na ya siku zote! Kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.“

VI
UNAPOLALA

1. Usiku ukija, kwanza ya kwenda kulala, twaa maji ya mbaraka, piga magoti, sali sala ya jioni.

2. Kêsha, nenda kulala, sema:

„Mungu wangu, nakupa moyo“

3. Hatta ukikawia kupata usingizi, sali tasbihi, umpe heshima Bikira Maryamu, uwaombee roho za Toharani.

6. MASHAURI MÉMA
I

Mtoto, usikae hapa Duniani kama nyama. Nyama hajui kusali, hajui kusoma, hajui adabu. Kula, kutembea na kulala, ndiyo kazi yake tu. Walakini, weye, Bin-Adamu, kumbuka roho yako na Mungu wako.

II

Mtoto, nikuulize kitu kimoja.

Utakaa hapa Duniani miaka mingapi, miezi mingapi, siku ngapi? —

Sijui —

Basi, Wataka kufanya nini katika maisha yako? — Kwanza, nataka kula. —

Vêma. Na baadaye? — Ntatembea. —

Na baadaye? — Ntalala. —

Na baadaye? — Ntalima —

Na baadaye? — Ntavuna. —

Na baadaye? — Ntafanya biashara, ntasafiri, ntapata mali. —

Na baadaye? — Labuda ntakuwa mtu mkubwa, ntapata heshima. —

Na baadaye? — Sherti ntakuwa mzee. —

Na baadaye? — Basi, ntakufa. —

Na baadaye? — Ntakufa . . . na kesha kufa . . . sijui mimi. —

— Hujui wewe, na mimi najua: kesha kufa, mwili wako utaoza kaburini, na roho yako itakwenda mbele ya Mungu.

Basi roho yako ikiwa safi, utapokewa kwake uwinguni, utakaa milele, usipate kufukuzwa tena.

Roho yako lakini, ikiwa na zambi, utatupwa

motoni kwa shetani, utakaa milele usipate kutoka tena.

Bin-Adamu, kumbuka mwisho wako; na mwisho wako, labda kesho!

III

Mtoto wangu, ukitaka kutenda neno baya, haya! waweza kujificha pahali watu wasipate kuona. Walakini utajificha wapi, usiku na mchana, usipo machoni pa Mungu?

Kimbia mwituni: Mungu yupo. Nenda baharini: Mungu yupo. Ingia jizani: Mungu yupo. Funga milango ya nyumba: Mungu yupo.

Basi, fanyiza killa neno lako, kama ukilifanyiza mbele ya watu; fanyiza killa neno lako kama katika mchana; fanyiza killa neno lako kama litaandikwa usoni mwako. — Bin-Adamu, kumbuka jicho la Mungu!

IV

Mtoto wangu, mpende Mungu wako zaidi ya mtu wowote, na kitu chochote, mpende jirani yako kama kupenda nafsi yako mwenyewe, kwa sababu ya Mungu. Ndiyo hiyo Sharia yote!

V

Mtoto wangu, neno hili unalotaka likutendewe

na watu, nawe liwatendee watu. Na hili neno usilotaka lisikutendewe na watu, wala weye usiliwatendee watu.

VI

Mtoto wangu, ukiingiwa na vishaushi vya shetani, tamaa mbaya, mawazo machafu, marra yatupie mbali, kama mate ya nyoka.

VII

Mtoto wangu, usiseme uongo. Uongo kazi mbaya.

VIII

Mtoto wangu, usiibe. Hatta sindano moja usiibe. Ukitaka kitu, mwombe mwenyewe: kana hataki, basi. Mali ya watu si mali yako. Kuiba hakuna mbaraka.

IX

Mtoto wangu, usifanye kiburi, wala uwivu, wala choyo, wala ulevi, wala hasira, wala uchafu. Mungu amekataza.

X

Mtoto wangu, shika adabu. Waamkie wakubwa wako, watukuze baba na mama, wasikilize watu wêma, acha watu wabaya.

XI

Mtoto wangu, usikose kusali, hatta siku moja. Umechoka? Basi, sali kidogo tu, walakini sali.

XII

Mtoto wangu, kumbuka unakaa katika watu wasiojua Mungu wala Dini: wakikuona weye mtu mbaya, watakufuru Mungu wako na Dini yako; wakikuona weye mtu mwema, watasifu Mungu wako na Dini yako.

XIII

Mtoto wangu, ukiwa mwana wa Kristu, usivunje mambo ya mwana wa Kristu.

7. SALAMU BORA.

1. Na jua hiamka,
   Marra ni kutamka:
   Tumsifu Yesu Kristu,
   Milele amina.
2. Nikingia kazi
   Nitasali wazi: Tumsifu ...
3. Hitwaa chakula,
   Naanza kwa sala: Tumsifu ...
4. Hija kanisani,
   Nanena moyoni: Tumsifu ...
5. Killa naanzalo,
   Wazo langu ndilo: Tumsifu ...

6. Kengele la kuchwa,
   Nainama kichwa: Tumsifu ...
7. Nendapo pumzika,
   Usiku natamka: Tumsifu ...
8. Na saa ya kufa,
   Mwisho ntoe sifa: Tumsifu ...
9. Kwisha vuta ńambo,
   Ningie na wimbo: Tumsifu ...
10. Milele niambe,
    Milele niimbe: Tumsifu.

P. S.

SEHEMU YA PILI

MIFANO

8. MWANA-FUNZI, KAMBA NA JIWE

Kijana mmoja alisoma elimu siku nyingi, asijue kabisa. Akafanya hasira, akenda zake, hatta kati ya njia akaona kisima, akenda kutezama kana pana maji anywe. Akaona jiwe la kisima limekatwa na kamba kwa sababu killa siku kamba hupita katika lile jiwe. Akasema: «Hii kamba imekata jiwe, sababu killa siku hupita, juu yake. Na mimi nitarudi kusoma: kwani, nikiwa mimi na moyo mgumu kama jiwe, na elimu ikiwa kama kamba, moyo utakatwa mwisho na elimu. Akarudi, akasoma, akawa mwalimu mkuu.

9. MACHUNGWA NA EMBE

Palikuwa na Machungwa
Chini
Ya mti,

Nayo yote yameoza.
Mtoto
Mdogo
Akaweka embe lake
Nayo
Hayo:
Likaoza vile vile.

10. MBWEHA NA MAZABIBU.

Mbweha alipita panapo chanja ya mzabibu, akaona kichala cha mazabibu meusi, mazuri mno. Akasimama, akamezea mate kwa tamaa ya mazabibu yale. Akainuka na kuchuchumia, akafunua mdomo, asipate kunyakua, kwani mfupi mno. Akaruka, akaruka, akaruka hatta kuchoka. Basi, akakata tamaa, akenda zake na kunena: «Mabichi!»

Mtu zaifu cheo asichoweza, huzarao.

11. USIIBE

Palikuwa na Panya,
Na kazi yake kucha
Kutafunatafuna
Maboga ya mtu mmoja.
Hatta mwisho
Akanasa na mtego.

Palikuwa na Nyani
Na yeye pia mwivi.
Hatta na siku moji
Watu wa mashambani
  Kuja basi,
Wakampiga risasi.
Haya, shauri langu
Hili: Mtoto wa Mungu,
Ukija 'tta usiku
Kula mali ya watu
  Utalia
Mwisho wako, kama nyani, kama panya!

12. KUNGURU NA MBWEHA.

Kunguru alipata kinofu, akaruka nacho, akatua katika kilele cha mti. Penye mti, kwa chini yake, palikuwa na mbweha: akamwona kunguru juu akasikia arufu ya kitoweo, akafanya tamaa nacho. Basi akamwamkia kunguru, akamwambia: «Jambo, jambo bwana angu!» Kunguru akainama, akamwona mbweha chini, akanyamaa. Mbweha akanena: «Ah bwana, ndege mzuri we! Sijamwona ndege mwenye urembo kamawe: rangi yaŋara, mkia mpana mfano wa upepeo, pambo la shingo, mdomo wa kunyoka sawa.» Kunguru akiinamiza kichwa kimya, akikubali. Mbweha akazidi kunena:

«Baki sauti. Sijapata kusikia; walakini haikosi kuwa ya uzuri kama umbo lako.» Kunguru asiweze kunyamaa zaidi, akafunua mdomo, akapiga: Kroa! Kroa! Kroa! Kinofu kikamchopoka, kikaanguka, kisifike hatta chini lakini: kikanyakuliwa na mbweha. Akabwakia, akenda zake.

Waswahili wa kale walinena: Haurambwa mkono mtupu. Maana ubembelezi si bure.

13. MBWA AKIMBILIAYE KIFANANI.

Mbwa alikamata kinofu, akaja, akapitia ulaloni juu ya mto ya maji maangavu, akauona majini mfano wa mbwa, ndiye ye mwenyewe, kinofu mdomoni. Basi akakiacha kinofu chake akarukia majini, kwenda kukitwalia kinofu kile. Basi, hapana wala kinofu, wala mbwa mwingine, na kinofu chake ye kimekwisha mpotea. Mkondo wavuta: asingekuwa mbwa, angezama.

Huonekana bin-Adamu wenye akili ya mbwa huyo, wakimbiliao kifanani, wakaliacha la kweli.

14. MZABIBU.

Kulikuwa mjini Mzabibu husema
«Umenipandisha
«Jù ya vyumavyuma,

«Ukanifungia
«Na makambakamba . . .
«Kwani? Sina nguvu?
«Nataka mahuru!»
Hatta siku moja, bwana, mkubwa wake,
Kafungua vyote.
Basi, katezame
Muti ule ule:
Masika yapiga,
Mzabibu wânguka,
Na, chini, matunda
Yote utopeni yameozaoza . . .

15. MBWIJI NA MWANA-KONDOO.

Siku moja mbwiji na mwana-kondoo walikutana kando ya kijito cha maji: mwana kondoo alikuwa amesimama, akitezama maji; mbwiji kaja nyumaye akashuka mtoni kwa juu kidogo, anywe maji. Akamwona kikondoo, akafanya tamaa ya nyama yake, akawaza sababu ya kumtakia vita, akamwambia: «Mbona ukayatifuatifua maji haya, ninywe matope?» Kikondoo kikaitikia: «Ee bwana, nawezaje kuyatenda mambo hayo? wewe juu huko mtoni, nami niko mbali kwa chini: mkondo wateremsha maji ya kwako, yanifikie mimi yasiweze

kurudi kwako.» Mbwiji akasema: «Ewe! Usubutuje kunywa maji kabla sijanywa mwenyewe?» Kikondoo kikaitikia: «Sikunywa maji, bado nanyonya maziwa ya mama.» Mbwiji akasema: «Basi, basi! Si weye uliyenitolea tusi mwezi wa sita huu? Kikondoo kikaitikia: «Haifay, bwana, sijazaliwa majira hayo: ni mwana wa miezi minne, tangu nilipozaliwa.» Mbwiji akasema: «Kama si wewe, hakosi ni baba wako, au mmojapo wa ukoo wako, sijui mimi. Nijuayo, ndiyo kama mmestahili kufa nyinyi nyote.

Akamrukia, akamrarua, akamtafuna pale pale, pasipo haki yoyote.

Wawi wamenena: «Mwenye haki ni mwenye kuweza.»

16. CHURA NA ŃOMBE.

Chura kimoja alitoka ziwa, aliingia mashamba, akamwona ńombe mnono, akamjongelea, amtezame dubwana hilo. Kimo chake chura hakikuzidi yay. Hayzuru, akawaza ataweza kujilinganisha na nyama kubwa. Basi, akajifurisha mbavu, akajifurisha, akamwuliza ńombe: «Dada, niangalie kama nimekupata unene.» Ńombe akaitika: «Bâdo kichura! — Ebu, dada? — Bâdo, nakwambia! — Hivi

tena? — Bâdo! bâdo hatta!» Chura akajifurisha, akajifurisha, hatta mwisho akapasuka, pa!

Ulimwengu umejaa watu wasio na akili zaidi ya chura. Watoto huigiza mazoezi ya watu wazima; watu wadogo hujifanya mabwana; killa mtu hujitaka makuu asiyoyaweza.

17. KIPEPEO NA NYUKI.

Kipepeo alikuwa
Akisema:
«E kumefanya kuzuri.
«Ee basi,
«Nitembee mimi shamba.»
Nae marra
Mama nyuki akajibu,
Juu ya mbuyu:
«E kumefanya kuzuri,
«Ndiyo kweli
«Nirukie mimi shamba
«Kuvunia!»

18. KITOTO NA KIOO.

Kitoto, asiyejua kioo bado, siku moja alifuatana na mamae mjini; aliingia sebuleni, alitezama kioo, akaona mfano wake katika kioo; akazani ndiye

mtoto mmoja wa mji. Akaona chuki, akatoa ulimi; nao mfano ukatoa ulimi; akamwonya ngumi, nao mfano ukafanya ngumi kwa ukali.

— Basi mtoto akaingia hasira, na kuanza kulia, na kutaka kupiga teke na ngumi katika kioo. Mamae, akitambua sababu ya hasira yake, akamwongoa, akamnyamaza, akamwambia: «Ewe mwana! si wewe uliyeanza? ukamtukana kwanza, nae akatukana; jaribu sasa mambo mengine. Waona: ukichekelea nae akakuchekelea; ukamkonyeza kwa mkono nae akakukonyeza; umekuwa razi, nae amekuwa razi.»

Mfano huo ndio mfano wa dunia: mtenda ovu, hutendwa ovu; mtenda mema, hupewa mema.

19. MTOTO NA PAKA.

Mtoto alipewa kitumbua. Kaja paka, kimsogea na kumtambalia, na kumbembeleza, na kufanya rororo, mkia juu. Mtoto akapendezewa, akammegea kitumbua kipande kizima, akampa. — Paka akadaka, akakimbia, asikubali kurudi. Mtoto akamtukana na kunena: «Ulikipenda kitumbua, hukunipenda mimi!»

— Ubembelezi si urafiki.

20. MAFUMBO.

Uvivu na njaa ni ndugu pacha.
Mtaka yote, hukosa yote.
Kazi isiyo kipimo, mwishowe watu huteta.
Heri adui mwerevu, kama rafiki mpumbavu.
Juzi na jana si kama leo.
Kawia ufike, kuliko kulala njiani.
Mambo taratibu humshinda mwenye nguvu
Ahadi ni deni.
Akili mali.

21. MBWA WAWILI WALIOSAFIRI PAMOJA.

Mbwa mmoja, jina lake Kondoo, kwa tabia yake kuwa ngema, aliingia njiani, kwenda safiri. Akakutana na mbwa mwingine, jina lake Mlizi, kwani mwenye ugomvi mno.

Kondoo akamjongea, akamwuliza: «Tumefuasa njia sawa, wapenda tusafiri pamoja? mwendo wa peke, kama wali usio na kitoweo.»

Waliponusana kidogo, na kukimbizana ovyo, na kuliana, mwisho wakapatana, wakashika njia, wakasafiri pamoja kindugundugu.

Wakenda, hatta wakafika mji moja. Mlizi akaanza kuwashambulia vita mbwa zote za mji huo, kufanya ukali, na kuuma. Kelele zikawa nyingi:

watu wakawatokea njiani wakawapiga fimbo na mawe, wakawainga mbali. Basi, safari ikavunjika vile: marafiki wakashika mbio, wakabagukana. Kondoo amepasuka sikio; Mlizi ana mguu mmoja na jicho.

— Haufay urafiki na mtu yeyote, usiyemjua kwanza.

22. MCHUNGA NYAMA.

Mtoto mmoja, jina lake Seki, alikwenda asubuhi kuchunga mbuzi na kondoo za baba. Hatta alasiri, asijue la kufanya, akawaza atawauzi watu bure. Akalia: «Chui! chui!» — Marra watu wote wamekuja mbio, kumtafutia chui, wamwulie mbali. Seki akawaendea mbele, akawacheka watu waliokuja kumletea shime. Wakavumilia wakanyamaa, wakarejea zao na haya yao. Hatta siku ya tatu, chui akaja, wala si chui urongo, ni chui kweli: akaliangukia kundi la nyama. Seki akimwona akalia: «Chui! chui!» Watu wa kijiji wakisikia wakasemeana: «Bado Seki huyo, na urongo wake!» Asiondoke hatta mtu mmoja. Chui akararua nyama kumi.

Aliyejulikana ni mwongo, ajaponena kweli hasikizwi.

23. NDAMA WA ŃOMBE, MBUZI NA KONDOO SHIRIKA NA SIMBA.

Zamani za kale, ndama wa ńombe, na mbuzi, na kondoo, ndio watu watatu, walifanya shirika na simba: «Hasara yetu moja; mali yetu moja. Apatacho yote mmojawapo, tugawanye.» Basi wakatega. Akanaswa mbawara katika wavu wa mbuzi. Marafiki wakaitana. Wakêsha timia pahali pamoja, simba akafanya hisabu kwa kucha zake, akahisabu: «Moja, mbili, tatu, nne. Tu wanne barabara. Haya, tugawiane mateka!» Wakamwitikia: «Ndiyo bwana.» Simba akamparura mbawara mapande manne. La kwanza akalikalia akanena: «Kipande changu mimi mfalme simba.» Akashika na la pili akinena: «Hiki sasa haki yangu.» Akashika la tatu akinena: «Hiki nakitwaa, cha mwenye nguvu.» Akatwaa na la nne, kwa kunena: «Hiki nakitaka; asiyekubali, ntamnyonga.»

Wako bin-Adamu namna ya simba: haki kwao ni nguvu.

24. PANYA WANA SHAÙRI.

Palikuwa na paka, jinale Mnyaku, hodari mno. Angekuwa paka wa pili mfano wake, wangekwisha panya zote. Hawaonekani, hawatoki kwa oga;

hujibanza ndani ya tundu zao, huwa na njaa kuu! Hatta siku moja ikaja habari Mnyaku amekwenda posa; zitatimia siku mbili asije. Ikapigwa mbiu, panya zote wakusanyike, waje baraza. Makombo yote, yapata labda panya kumi na mawili wakawapo barazani kwa shauri. Buku mzee, mwenye mvi, akakaa kitini, akanena: «Hatari yetu kubwa! Au tufe kwa njaa, au tufanye hila. Ajuaye ya kufanya, aseme.» Wakaitika «E!» Walakini hapakuwa mtu aliyefunua mdomo tena. Mzee buku akanena: «Shauri yangu ninayo moja, ndio, tumfunge Mnyaku mbugi mguuni: akienda pahali, tusikie din, din, din yake, tukimbilie tunduni.» Panya zote wakaitika: «Ngema mno shauri yako; ni akili hiyo, yatosha!» Mzee buku akanena: «Haya basi! tumteue mmojawapo, tumtume kwa hiyo shuruli.» Ndipo mgogoro: panya zote kwanza walikubali shauri kama mtu mmoja; sasa hapana mtu! Mmoja akanena: «siendi, sina wazimu.» Mwingine akanena: «Haifay!» Mwingine akanena: «Siwezi.» Basi wakabagukana!

— Kusema, si kutenda!

25. MTUMBIRI RALANI.

Mtumbiri, alipo juu ya mti uliosimama karibu na rala, akaona teo iliozibuliwa ukutani, akasogea,

akachungulia ndani, akaona vyakula tele, tele, loo! nakosa kutaja... mapera, ndizi, embe, koma-manga, nanasi, mapapay, njuguu, maandazi, sukari, asali, maziwa. Mlango umefungwa, madirisha yamezibwa, na mwenyewe hapana. Mtumbiri akajipenyeza ndani, akauangukia mkungu wa ndizi, uliotundikiwa pale pale. Akaonja ndizi, akaonja asali, akaonja pera, akaonja muwa, akaonja maandazi, akaonja akaonja! Hatta mwisho akafanya lepe la usingizi, akalala. Marra mlango wakwaruza, ndiye mwenyewe aliyefungua, ajaye kukagua. Mtumbiri akataka kukimbia: tumbo zito la kujaa, hakufaa kupita teoni, akabanwa. Panya akimwona hatarini akamwambia: «Uliingia tumbo la njaa, hutoki isipokuwa ukonde kwanza.

Aliyonena panya, namwambia mwivi: «Mali ya watu imekushika mpaka ulipe!»

26. MAFUMBO.

Hakuna refu lisilo ncha.
Hakuna kubwa lisilo ukomo.
Maneno si kitendo.
Asiye akili, sifuatana nae,
Maji yaliyomwagika hayazoleki.
Saburi yavuta heri.

Apataye, si mwenzio,
Jogoo la shamba haliwiki mjini.
Nenda pole ufike.
Mpanda ngazi hushuka.
Haraka haraka haina mbaraka.
Mtu mbaya, rafiki hana.
Mpenzi hana kinyongo
Mtenda mêma, avuna nêma.

27. PUNDA NA ELIMU.

Mtu mmoja alikuwa na punda, alimfundisha mambo ajabu. Kwanza ilikuwa kazi ngumu sana kumsomesha punda: haikwenda, ila kwa bakora. Hatta mwisho kidogo kwa kidogo, nyama akazisikia akazitii amri zote. Ya kwanza ageuke asalimu kuume, ya pilí ageuke asalimu kushoto; ya tatu apige kwata moja chini, maana «Naam»; ya nne apige makwata mawili, maana «La»; na vivi hivi.

Alipohitimu, bwanae akamtatia kilemba cha mwalimu: ncha za masikio asipate kuzifunika zilitokeza kidogo. Ikesha akamfungasa nyumaye akamtembeza mjini, awaonye watu elimu ya punda, apate tuza.

Saa ya kwanza mambo yakamwongokea vizuri, watu wote wakitokea, wamtezame punda, kiroja

gani! Haikutimia saa, bwana, kwa kuchoka ao kwa kusahao akadanganyika, hakuzifuliza amri mfulizo wa desturi. Basi ikawa porojo; bwana akiamuru «Naam», punda akiinama, akiamuru «inama» punda akilialia; hatta akiamuru «Tuonye mwali aliye mwana mtulivu», punda akasogea, akenda, akisimama mbele ya kitwana kibarango. Ikatosha: marra watu wakaruka, wakamzomea na kulia: «Rudi chuoni! rudi chuoni! mbio! mbio!»

— Elimu isiyo na akili kichwani, elimu ya kasuku, si elimu; yapiga zomeo. Elimu si kusoma chuo tu, ni kuelewa.

28. VITENDA-WILI.

— Gumu-gumu huzaa teke;
Teke-teke huzaa gumu. (ɪpuɪɣɐɯ)

— Nikitupa mshale wangu mchana huenda mbali
Nikitupa usiku, huenda karibu. (oɥɔɪʃ)

— Waana watatu: akiondoka mmoja wawili hawafay. (ɐƨɣɐɯ)

— Mtoto wangu killa mwaka hulala chini. (ɐƨoq)

SEHEMU YA TATU.

29. UPEPO AO HAWA.

Mtu ataka upepo, apate kukaa mzima: pasipo upepo, hufa. — Basi, tunakaa, tunakwenda, tunalala ndani ya hawa au upepo vile vile kama samaki hukaa ndani ya maji. Hatta nyama, hatta miti hutaka hawa; hatta moto hutaka hawa; tusipo na hawa, hatuwezi kuwasha moto.

Basi, upepo huo mwinyi kutufaa kabisa ni mapaji ya Mungu.

30. MAJI.

Watu na nyama wangekuwa hawana maji, wangefanyaje? Hatta miti yasiyo na maji hufa.

— Maji hufaa kunywesha watu, nyama na miti; hufaa kuosha ua kufua nguo; hufaa kupika chakula.

— Hatta maji mengine yana chumvi; yakikauka chumvi yasalia.

— Si basi, maji ya bahari, ya vîziwa, ya mito yafanya ukungu, na ukungu wapaa kama moshi,

wageuka mawingu. Tena mawingu yale yafukuzwa na pepo, yageuka mvua, yafanya maji marra ya pili. Na mashamba yetu yakipata maji hayo yaota majani, na miti, na mboga, na mtama, na muhogo, na muhindi, na viazi, na matunda, vyakula vyetu.

Maji pia ni mapaji ya Mungu.

31. MOTO.

Moto hukaa katikati ndani ya nchi: hatta vilima viko (kama kule Ungazija na Boribo na Kirunga) vinyi kutoa moto juu, Moto hukaa pia ndani ya mawe, ndani ya miti, ndani ya vibiriti.

Basi, tunawasha moto nasi, tupike, tule; tunawasha moto, tuyeyushe chuma, tufulie vyombo kama visu, na majembe, na mashoka, na mundu, na panga, na mikuki, na mishale, na masango, na mapete, na minyororo, na funguo, na saa, etc.

Moto pia ni mapaji ya Mungu.

32. CHUMA, SHABA, RISASI etc.

Udongo wa nchi unazo mali nyingi. Unayo mawe ya kujenga nyumba; unacho na chuma cha kufuliwa vyombo; unayo na risasi, na shaba, na feza, na zahabu, na vitu vingine vya killa namna.

Hayo yote pia ndiyo mapaji ya Mungu.

33. MITI.

Mungu amepanda majani na miti mingi, watu wayatumie.

Miti mingine chakula chetu, kama mboga, muhogo, mtama, muhindi, viazi; mingine huzaa matunda matamu, kama mwembe, mfenesi, mpapay, mpera, mgomba wa ndizi, mnazi; mingine huleta chakula cha nyama zetu, kama majani ya mashambani; mingine ni dawa zetu; mingine huleta mafuta; mingine huleta uzi wa kufanya kamba na nguo; mingine huleta rangi ya killa namna; mingine huleta maua kwa uzuri; mingine hufaa kuni za kuwasha moto, hufaa mbao, na boriti, na fito za kujenga, kuunda vyombo na markebu, kufanya masanduku, meza, vinu, viti, na kazi ya killa namna; na miti mingine ni magugu matupu.

Miti na majani mapaji ya Mungu.

34. NYAMA.

Nao nyama wamewekwa wawatumikie Bin-Adamu.

Vidudu vingine hutuletea dawa, vingine hariri, vingine asali, Samaki ni chakula chetu. Ndege, na mbuzi, na kondoo pia chakula. Punda, farasi, ngamia wachukua mizigo yetu. Ñombe atuletea

nae maziwa yake, nyama yake, ngozi yake, pembe zake, kazi yake.

Pana nyama wengine wakali, kweli: ndiyo simba, chui, nyoka; na vidudu wengine waharibivu, kama mchwa.

Basi, Mungu ameyaumba hayo yote, tusipate, sisi Bin-Adamu, kukaa katika uvivu wetu, tufanye kazi, tulime, tuvumilie, hivyo tumtumikie Mungu, tuende kwake kustarehe milele.

35. MAFUMBO.

Muumwa na nyoka,
Akiona kamba, hushituka.
Mwenye kutenda mêma;
Ajifanyizia mwenyewe.
Mwenye chake,
Hakosi cha mwenziwe.
Asisikie la mkuu,
Huvunjika mguu.
Habari ya uwongo ina ncha saba,
Habari ya kweli ina ncha moja.

36. MNAZI.

I

Mnazi ni mti wa namna ya mchikichi, na mvumo, na mkoche, na mkindu, na mwale, na mtende, na mpopoo. Maana ni mti usio na majani ya kufanana na majani ya miti iliyo aina ya mwembe, na mgomba, na mpapay, na mpera, na miti mingineo umbo lao sawa: una m a k u t i basi.

Kuzaa kwake kungine pia. Kwanza hutunga mimba ya k w a r a r a: jinsi yake kama muhindi. Kwarara likipasuka, latoa k o l e: kole, watu wengi wasema t a w i. Kole likachanua, likafanya m a u a.

II

Maua yaliyopangiliana mfano wa mpunga, yameitwa u p u n g a: hayazai, ni madume tu. Maua yenye kuzaa, ndiyo majike, yamekaa moja kwa moja chini ya vitawi, yamekuwa vidonge, yameitwa v i d a k a. Kidaka kinakua, kinaanza kutunga maji, kinakuwa k i t a l e. Kitale kinakua, hatta kimevimba sana, kimejaa maji mazuri ya kunywa, kimepakwa ndani u r a m b e - u r a m b e wa kukomba, ndicho chakula kitamu mno: si kitale tena, huitwa d a f u. Dafu likesha kua zaidi, hatta lina-

sukasuka ndani, kwa maji kupunguka, ndipo liitwapo koroma: maji yake yamekwisha pendeza. Nyama ikesha kuwa ngumu ndani, si koroma tena, ni nazi. Nazi ikikauka makumbi, ikififia rangi kabisa, yaitwa mbata, yafaa kuanguliwa.

III

Nazi, ukiipasua sawasawa kwa upande, kwanza waona makumbi yake kwa njye: nyuzi tupu, unene wapata nyanda mbili tatu. Makumbi yamekifunika kifuu: nacho cha mti mgumu mgumu, umbo la yay. Juu kimechongeka pembe tatu; kwa chini, upande wa kikonyo, kina tundu tatu. Tundu ndicho ḳitovu pa kuungana mtoto na mamae kwa chango la uzazi: mama ndio mnazi, mtoto ndicho kiini chenye kilicholala na kuzama ndani ya nyama ya nazi. Asiye na maarifa, hapati kukigundua kiini hicho, kwa kuwa kidogo sana, kimefumbika. Wakati wa kuipanda nazi, kiini kitakuwa mche; nao mche utatokeza penye mojapo ya tundu zile tatu, kwisha penya katika nyama iliyoenea mote mnamo nazi. Nyama hiyo ndiyo sawa yake ute wa yay. Kama vile ute wa yay waliwa na kinda asijetoka, vile vile nyama ya nazi huwa chakula cha kiini majira ya kutoa mche.

IV

Katika nchi yetu, ziko mbegu mbili za mnazi: kuna mnazi mkubwa wa mashamba; kuna na mnazi wa ki-Pemba (kitamli), nao mdogo punde, mwembamba zaidi, nazi yake rangi ya kimanjano. Mnazi wa ki-Pemba hupandwa hassa katika bustani, na karibu ya nyumba za watu: madafu yake yapendeza mno, hunywewa yote, yakasazwa machache kupata kuwa nazi mbivu. Mnazi wa mashamba, wa kukua sana, zaidi ya mnazi wa ki-Pemba, namna yake mbili: mmoja una magubi na nazi kufanya rangi ya kimanjano kidogo, kama mnazi wa ki-Pemba; wa pili magubi yake na nazi zake chani kiwiti tu.

Mnazi, asili yake upande wa maawio ya jua, visiwa vya Oseania. Kwa sasa lakini umepandwa katika nchi nyingi: wastawi katika nchi ya hari na mnyevu.

V

Mnazi hukua sana, têna hukua upesi. Mwaka wa tanu tokea kupandwa, waanza kuzaa. Wapenda kulimwa: mnazi uliopotea katika nyasi, au katika magugu, hauzai sana, haufani.

Urefu wake waweza kupata mikono sittini. Shina

DUQUESNE UNIVERSITY LIBRARY

lake lafanya kitumbo kidogo kwa chini; baadaye gogo lake lasimama moja kwa moja, hatta ncha yake penye kutanda makuti. Mna kilele kati: kimetungwa na madifu, iliyo mfano wa nguo ya kufumika. Kilele kilipokwisha pasua madifu, chachanuka, chatoa makuti. Makuti machanga husimama juu pamoja; makuti mazima hutapakaa kwa chini kabisa. Wa-mvita wana fumbo:

Kumbi fu lambile biti:
Kimbele-mbele waume!
Kiumbe mwanzo hajuti;
Majuto huja kinume.

Maana, wazee huwaambia vijana: «Mwaingia njiani; nendeni basi, mkiona upya na uzuri tu; msiowaza mambo mutakayopata mbele. Mwisho wenu ni kukonga kama siye, ni kufa.»

Beina ya makuti mawili patokea kwarara. Makwarara ndiyo hayo wachezeayo watoto wakifanya madau. Kwarara latoa kole la maua, ndilo tulilosema kwanza.

VI

Mnazi una mafaa mêngi; tuhasibu basi:

1) Maji ya kunywa, katika dafu.

2) Tembo. Mgemi hushika kotama lake, huvuaza kwarara changa lisijefumuka bado, akalifungia kibuyu. Machozi ya kwarara lililokatwa ncha hutonatona mnamo kibuyu; akaja mgemi siku ya pili, akamimina kibuyu katika buyu, akapata tembo la tamu. Tembo likiachwa siku moja katika buyu, lachacha kidogo, lafanya tembo halisi. Tembo likichacha siku tatu lakua kali zaidi, laitwa chizi.

Tembo huwa na kileo: mwajua fumbo: «Riziki za wagema mikononi mwa walewi.»

3) Siki. Tembo likiachwa ṣana, hatta likachachuka kabisa, lafanya siki: ndiyo siki ya tembo.

4) Asali. Tembo la tamu likipikwa, likakawishwa motoni, lakuwa asali; ndiyo asali ya tembo, au asali ya ngizi.

5) Tui. Hukuna nyama ya nazi kwa mbuzi. hupata chicha. Chicha zikikamuliwa, hutoa tui; baki machicha wanayokula kuku. Tui la nazi lachujiwa kwa kuńuto au kwa kifumbu: lafaa kupikia wali.

6) Mafuta. Nazi hufuliwa kwa kifuo au muo, hupasuliwa vizio viwili, hukopolewa nyama; nyama ikaanikwa, ndiyo kopra. Kopra hushindikiwa mafuta. Baki machicha au shudu. Mafuta ya

nazi yana matumizi sana, ya kuwasha taa, ya kutia katika karahana; ya kufanya sabuni; mafuta mapya huliwa, mêngine hutengenezwa, yakawa kama siaji, ndiyo yaitwapo Margarin.

7) Urambe-urambe. Nyama ikiwa haijaganda sana dafuni, huwa tamu mno, huliwa: ndio urambe-urambe.

8) Nazi. Nyama ya nazi ikesha gandamana na kuwa ngumu, huwa na mafuta sana, hutafunwa vivi hivi. au huchunwa, hupikwa kwa asali.

9) Joya. Nyama ya mbata iliyoanza kumea, huitwa joya: huliwa. Joya nalo tamu mno.

10) Kichilema. Kichilema ndio moyo wa mnazi. Moyo upo chini ya kilele: huliwa kama mboga.

11) Kamba; zulia; barashi etc. Makumbi yaliyofuliwa katika nazi hutumika jinsi nyingi: husokotewa kamba, hutengenezewa zulia, burashi na vitu vingi.

12) Makuti. Makuti yana matumizi namna kwa namna: ya kuezekea paa (makuti ya kiungo, makuti ya pande); ya kuzungusha boma (makuti ya komba); ya kusuka mapakacha, etc.

13) Ununu. Gome la gubi, lile la juu lafaa kama kamba: laitwa ununu.

14. Uchukuti. Uti wa kati ya ukuti, huitwa

uchukuti: husukiwa makuñuto, na majamanda na matunga, etc.

15) Utembwe. Uzi wa ukuti waitwa utembwe au kifumuwale: wafaa.

16) Kifuu. Kifuu kina matumizi bora. Kwisha tengenezwa, kinakuwa kikombe; kinakuwa mwiko; kinakuwa mkakasi; kinakuwa chochote. Pia chakatwa vipande, chakerezewa vifungo.

17) Mti. Mti wa mnazi wafaa kuzuilia udongo kama kizingiti mteremkoni; kama nguzo ya kupanda kando ya mto.

VII

Zamani za kale kwa Wa-Greki, mwenye kuwashinda wenziwe katika machezo hupewa kuti bichi, hutembezwa mjini kwa shangwe: kuti lilikuwa alama ya ushindi.

Hatta leo kwa Wazungu, mtu akiambwa amepata kuti, ndio msemo wa kunena: ameshinda, ikiwa katika mchezo, ikiwa katika vita, ikiwa kuwapita wenziwe jinsi yoyote, kwa uhodari, kwa elimu. Toka zamani sana basi makuti yana heshima: hupambwa njiani, ukutani, majira ya sikukuu, majira ya matembezi ya shangwe. Rabbi 'etu alipoingia Yerusalem, kwa shangwe la watu, wali-

msindikiza wakichukua makuti ya mtende kwa ajili ya kumfanyizia heshima. Mashahidi wa dini hupichwa picha yao na kuti moja mkononi; maana ya kuti hilo: sababu wakamshinda shetani, siku walipomwaga damu yao kwa uhodari, kuliko kukana dini ya kweli.

37. MAFUMBO.

Aliye kando, haangukiwi na mti.
Akataaye itwa, hukataa aitiwalo.
Asiyekiri ushinde, hakuwa mshindani
Usipoziba ufa, utajenga ukuta.
Mwana umleavyo ndivyo akuavyo.
Kimya kingi kina mshindo mkuu.
Asiopo, na lake halipo.
Mchea mwana kulia, hulia.
Liwalo lolote, na liwe.
Maji yaliyomwagika, hayozoleki.
Mtaka cha mvunguni, huinama.
Kulla mlango una ufunguo wake.
Mapenzi hayana mâcho.
Mchovya asali hachovyi marra moja.
Chema chajiuza, kibaya chajitembeza.
Akili nyingi huondoa maarifa.
Dua ya kuku haimpati mwewe.

SEHEMU YA NNE.

38. AYUBU.

I

Zamani za Yusuf palikuwa na mtu mshenzi, mchaji wa Mungu, jina lake Ayubu, wa kizazi cha Esau. Nchi yake bara Arabu kaskazini. Ni mtu amini, karimu. Mwiny'ezi Mungu alimwongolea mâmbo yake: ali na watoto wâna-ume saba, wâna-ake watatu; mali zake nyingi: ana watumishi wêngi; ana kondoo sabat'alaf; ana ngamia ṣalaṣat'alaf; ana ṅombe alfu, na punda hamso-mia. Watu wote walimpenda, wakimwona mtu wa ibada, mwinyi haki, mwema sana kwa maskini.

Basi Shetani humwonea, hatta siku moja akataka ruhusa kwa Mungu kumjaribu.

II

Basi siku moja watoto wa Ayubu walifanya karamu kwa kaka yao; Ayubu yupo nyumbani kwake; akamjia mtu mmoja, akamwambia: «Tulikuwa sha-

mba siye wakulima wako, ńombe wakilima, punda wakila majani; basi Wasaba wakatushambulia marra, wakanyanganya ńombe na punda, wakaua watu wote, ila miye peke yangu nikakimbia, nimekuja kukwambia.» Hajêsha kusema huyo, amekuja mtu wa pili, anasema: «Radi imepiga kondoo zako pamoja na wachungaji; wote wakateketea, ila peke yangu mimi nikaokoka, nimekuja kukwambia.» Hajêsha na huyo, anaingia mtu wa tatu: «Wakalde wamechukua ngamia zako, wakaua watu wote, ila peke yangu mimi nikakimbia, nimekuja kukwambia.»

III

Basi Shetani alimjaribu Ayubu bure, asipate kumkosesha. Akazidi kumtakia uovu, akamtesa mwilini mwake, akamweneza madonda mwili mzima.

Maskini Ayubu alikaa ndjye katika jaa, akishika kigae akipangusa usaha. Mkewe, asiweze kuvumilia usaburi wake, akamwambia kwa uchungu: «Je! Upumbavu wako haukuachii? Mtukane Mungu, ufe.» Mwenyewe lakini akamjibu: «Maneno yako ya kike kijinga. Kama tumepewa mêma kwa Mungu, kwani tusipokee na mateso?»

IV

Wakamjia na marafiki wake watatu kumwangalia, kutaka kumtuliza moyo. Kwanza wakakaa nae siku saba, wakimwangalia tu, wasiseme neno, jinsi walivyomsikitikia, kwa ṣababu ya mateso yake kuwa mêngi. Mwisho wakazani ana zambi, ndiyo maana ameazibiwa na Mungu; wakataka kumwonya shauri atubu, amnenyekee Mungu, apate kuondolewa na kuponywa. Ayubu lakini alijua ṣivyo, ila Mwiny'ezi Mungu hutenda atakavyo: mtu mkosi humwazibu; mtu amini humjaribu. Akijaribiwa mtu mchaji wa Mungu, sivyo kwa azabu, ila kwa sababu ya kumstahilisha na kumtakasa zaidi. Akawajibu: «Nihurumieni, enyi marafiki wangu. Mkono wa Mungu umenielemea, nanyi mwanisumbua! Walakini najua mimi: Mkombozi wangu yupo kweli. Nitafufuka mwisho: ngozi yangu itarudi juu ya nyama na fupa. Nitamwona Mungu wangu, miye mzima kwa mwili wangu, wala si kwa kivuli tu; nitamwangalia kwa macho yangu. Matumaini yangu yatosha kunituliza moyo.»

V

Mwisho marafiki wake wakashindwa, wakaungama, wakamwomba razi. Naye Ayabu hakuvu-

milia bure, akapata baraka: Mwiny'ezi Mungu akamponya, akampa mali kawili.

Ayubu akazaa watoto wêngine, wâna-ume saba, wâna-ake watatu; akastarehe miaka mia u arbaini, akaona wajukuu wake, na vilembwe, na vilembwekeze, hatta, alipopata umri wake miaka miateini u ashara, akafa.

39. DAUDI AMWUA GOLYAT.

I

Nyuma hapo Wafilistini wakaja na vita. Mmoja wao mdubwana akatokea mbele za askari, akawaelekea Waisrail, akawaambia: «Siyo nyinyi watumwa wa Saul, na mimi Mfilistini? Basi mchagueni mtu mmoja kwenu, aje hapa, tupigane mimi naye. Akinishinda, akiniua, sisi tutakuwa watumwa wenu; nikimshinda, nikimwua, nyinyi mtakuwa watumwa wetu.» Jitu lile, jina lake Golyat; urefu wake mikono sita na nyanda nne; ana kofia na koti za shaba; amechukua ngao ya shaba; uti wa mkuki wake jiti zima kama mchi. Basi siku arbaini killa siku asubuhi na alasiri, akatokea mbele za Waisrail, akamtaka mtu kushindana nae. Hakusubutu hatta mmoja, jinsi walivyotishwa.

II

Siku za hapo Daudi si askari bâdo, kwani kijana sana. Ndugu zake watatu walikuwa lakini pamoja na askari: akaja siku moja kuwaangalia. Alipokijizungumuza na nduguze, akamwona Golyat ametokea mbele, akiwatukana Waisrail, asisubutu mmoja kumwendea kupigana nae. Akaambiwa mfalme, ameona haya sana, hatta ameapa, mwinyi atakayemshinda Mfilistini huyo, atampa mali nyingi, atamwoza mwanae. Daudi akawaacha nduguze, akamwendea Saul, akamwambia: «Miye mtumwa wako nitakwenda, nitapigana na Mfilistini.» Saul akamjibu: «Huwezi kushindana na Mfilistini huyo: wewe mtoto, naye ni mtu mzima, mzoevu wa vita tangu ujana wake.» Daudi akaitika: «Nalipochunga kondoo za baba'angu, simba akija, akimchukua kondoo mmoja, mimi hufukuza, humkomboa kondoo, simba humsonga shingo, humwua. Basi Mfilistini huyo nitamwulia mbali kama simba. Rabbi, aliyeniopoa katika makucha ya simba, ataniopoa katika mikono ya Mfilistini.» Saul akajibu: «Haya! Rabbi akusimamie.»

III

Saul akatwaa koti yake ye ya shaba, akamvika Daudi; akatwaa na kofia ya shaba, akamtia ki-

chwani; akampa na upanga wake mwenyewe mkononi. Basi Daudi akajendea mbele kidogo, asiweze sana; kwani hakuzoea. Akaona siyo kumfaa, akavua koti na kofia, akaacha na upanga, akatwaa bakora yake, akaondoka. Akashuka bondeni, akachagua mbwe tanu zilizoviringana, akazitia mkobani, akafunga kombeo tayari mkononi. Akatokea kati ya Waisrail na Wafilistini, akamkonyeza Golyat kutaka kupigana nae. Golyat, alipomwona kijana huyo, akamchukia, akamwambia: «Je! Mbwa miye, uje kutaka kunipiga bakora? Jongea, nikuulie mbali, niwalishe nyama na ndege kwa mzoga wako.» Daudi akamwitikia: «Wewe unanijia mwinyi upanga na mkuki na ngao; mimi ninakujia kwa amri ya Mungu, ndiye Rabbi ya askari wetu, uliowatukana leo.» Mfilistini akimjongea, Daudi upesi akatia mbwe moja katika kombeo, akazungusha, akapiga, akampata Mfilistini barabara katika panda la uso: Golyat akaanguka kifudifudi. Daudi akamkimbilia, akachomoa upanga wake Golyat katika ala, akamkata kichwa. Basi Wafilistini, wakiona mkubwa wao amekwisha kufa, wakafanya woga, wakavundjika, wakaanza kukimbia. Waisrail wakawaandamia mbio, wakawafukuza, wakawaua wengi, wakawashinda kabisa.

40. ABU-SALUM MWANA WA DAUDI.

I

Mfalme Daudi alianza kwa kuwa mtu wa fazila. Illakini hakuwa na imara: alipokwisha kuwashinda maadui, akajivuna, akapungua siku kwa siku; hatta mwisho akatenda zambi mbili kubwa sana. Kwanza akamchukua Betsabe mke wa Uria; ya pili akatoa amri Uria aponzwe mbele za maadui, penye mashindo kuwa makubwa, apate kuuawa. Mwiny'ezi Mungu akamkasirikia Daudi akampeleka Natan, Nabii, amwonye zambi zake. Daudi akatubu, akaondolewa zambi; walakini akapashwa azabu.

Azabu yake, mwana aliyempata kwa Betsabe ndiye mke wa Uria, akashikwa na ugonjwa, akafa udogoni. Baadaye, mwanae mkubwa, Abu-Salum akamwase, akafanya fitina.

II

Abu-Salum, umbo lake zuri: toka miguu hatta kichwa alikuwa na utimilifu wa maungo yake yote; wala hapana mtu yeyote aliyemshinda uzuri katika raya zote za baba wake. Ilakini tabia yake ilikuwa na upungufu, alifanya kiburi, alishikwa na tamaa ya makubwa.

Killa siku asubuhi, alikuja akisimama pande za

baraza; akiwaona watu wamekuja kutaka haki kwa baba, huwaambia: «Kisa chako kisa chema; wa-«lakini watu wa mfalme hawatakusikia. Laiti kama «ningekuwa mfalme mimi, ningewafanyizia haki watu wote.» Akimjongea mtu kutaka kupiga magoti mbele yake, mwenyewe humshika mkono akibusu.

Hutenda vile, kusudi yake kuwapendeza watu. Hatta alipoona amekubalika katika nchi yote, akataka kumwondoa baba katika ufalme aingie mwenyewe pahali pake. Akaanza kuwafitini watu, akawapa silaha, akaja na vita kumshambulia baba.

III

Daudi akasikitika mno, akakimbia nambo ya mto Yordani, akatengeneza vita, apate kumzuia Abu-Salum. Siku walipoondoka askari zake kwenda kupigana na Abu-Salum, Daudi akawaambia maakida, hasa Yoab, mkubwa wao: «Msimpige mwan'angu Abu-Salum; ila mkimpata, mkamlete salama!»

Mapigano yakawa na nguvu, hatta Abu-Salum akashindwa, akakimbia mbio kwa punda. Hatta punda alipopita chini ya mti mnene, Abu-Salum akakamatwa kwa nywele zake katika matawi; punda akamchopoka, mwenyewe akaniñinia kwa nywele zake, zilizotatiana katika matawi.

IV

Askari za Daudi wakamfumania Abu-Salum wakamwita Yoab. Yoab asiweze kumvumilia mwana huyo mbaya, akamchoma kifuani mikuki mitatu. Askari wakamwangusha chini, wakachimba shimo kubwa, wakamzika pale pale, wakakusanya chungu kizima cha mawe juu yake.

Mfalme Daudi aliposikia habari kwamba mwanae amekufa katika vita, akaona sikitiko kuu, akamlilia sana, kwani mwana; akasema: «Abu-Salum, mwan'angu! Laiti ningekufa miye! Mwan'angu Abu-Salum!»

41. MAFUMBO YA MFALME SELEMANI.

1. MUNGU

1. Hekima, mbeleye ni uchaji wa Mungu. *Mafumbo 1, 7.*

2. Rabbi apeleleza mwendo wa Bin-Adamu; nyayo zake azivumbua ndjiani. *Mafumbo V, 21.*

2. SALA

3. Fahamu Muumba wako, kwamba uli kijana; wala usikawie mpaka zitakuja siku mbaya ao kwa masumbuo ao kwa uzee, utakapoona uchovu. *Mashauri, XII, 1.*

3. KUTUBU

4. Mficha zambi zake hataongoka; ila mwinyi kuungama na kuziacha ataonewa huruma. *Mafumbo XXVIII, 13.*

4. WANA NA WAZEE WAO

5. Aogopaye kutumia fimbo amtakia mwana maovu; mpenda mwana amtia adabu na mapema. *Mafumbo, XIII, 24.*

6. Fimbo na maonyo ya adabu mbegu yao hekima: mwana mfuata mapenzi yake humtilia haya mamae. *Mafumbo, XXIX, 15.*

7. Mpumbavu huchoka magombezo ya baba, ashikaye maonyo ni mwerevu. *Mafumbo, XV, 5.*

8. Mwana, yasikize mafundisho ya baba, wala siyapuze maonyo ya mama. *Mafumbo, I, 8.*

9. Mwana mwema furaha ya baba; mwana mpotofu sikitiko la mama. *Mafumbo, X, 1.*

10. Mwana umleavyo, ndivyo atakuwavyo. Atakapokuwa mzee, mwendo wake ni huo bado. *Mafumbo, XXII, 6.*

11. Mwiba cha baba na mama, anambiaye si zambi, na muua bin-Adamu hali ni moja. *Mafumbo, XXVIII, 24.*

5. ELIMU NA KAZI

12. Mvivu wa kujifunza atapatikana na mabaya. *Mafumbo, XVII, 16.*

13. Elimu na tartibu ya mtu humletea mwenyewe bahati. *Mashauri, VII, 13.*

14. Bora kijana maskini akiwa na hekima, kuliko mfalme mkongwe na mwinyi wazimu asiwaze mambo ya kecho. *Mashauri, IV, 13.*

15. Pafanywapo kazi, pana wingi; papigwapo midomo kutwa, pana ndjaa killa marra. *Mafumbo, XIV, 23.*

16. Mlima konde lake, atashiba vyakula; mpiga uvivu mpumbavu mkuu. *Mafumbo, XX, 11.*

17. Ee mvivu, kawaangalie siafu watendavyo, upate ku-

fundishwa. Wajapokuwa hawana mkubwa wao, wala msimamizi, wala mkufunzi, waweka tayari vyakula katika siku ngema, wakusanya kande wakati wa mavuno. Ee mvivu, utakoma lini kulala? Utaamka lini? Wanena: nilale kidogo bâdo, nisinzie marra moja, nikundjue mikono kidogo tu nipate kupumzika; na vivyo siku zote, mpaka uingiliwe na ukiwa kukutokea kama msafiri, mpaka ushikwe na umaskini, rafla yake kama ya adui na mata. *Mafumbo, VI, 6—11.*

42. WAFALUME YOSAFAT NA AKAB.

I

Zamani za Nabii Ilias, katika ufalme wa Yuda palikuwa na mfalme aitwaye Yosafat, mtu mwema, mchaji wa Mungu. Yosafat huwafanyizia haki raya zake zote, huwakataza wasifanye sanamu kuziabudu: akampendeza Mungu, akaongokewa mambo yake yote.

Katika ufalme wa Israil, palikuwa na mfalme aitwaye Akab, mtu mbaya, asiyemcha Mungu. Mfalme Akab alimwoa mke wa kishenzi, ndiye Yezabel, binti-sultani wa Tir. Basi akaiabudu miungu ya mkewe, ndiyo miungu ya Tir, mmoja aitwaye Baal, wa pili aitwaye Astarte. Akataka raya zake waiabudu miungu hiyo ya uongo, akawatenga na ibada ya Mungu wa kweli, akawaambia: «Baal, ndiye mungu wenu!»

II

Palikuwa na mtu, jina lake Nabot, mwinyi shamba lake la mizabibu limepakana na nyumba ya Akab. Basî mfalme akamwita Nabot, akamwambia: «Niuze shamba lako, nipate kufanya bustani. Nitakupa shamba jingine la mizabibu pamoja na feza kadiri utakayo.» Nabot akaitika: «Siuzi shamba, kwani shamba la wazee wangu.» Akab akafanya uchungu. Akaulizwa na mkewe Yezabel sababu ya uchungu wake nini, akamwambia. Mkewe akamtuliza, akawaita watu waovu faraga, akawaambia wamchongee Nabot uongo, apate kumpoteza. Wakamchongea, wakanena: «Ametukana Mungu; ametukana na mfalme.» Nabot akahukumiwa afe, akapelekwa kiungani kwa mji, akatupwa mawe, hatta akafa: mbwa wakaja, wakalamba damu iliyomwagika chini.»

Akab akatwaa shamba la Nabot. Basi Mwiny'ezi Mungu akamwonya Ilias amwendee Akab, ampatilize. Ilias akamwambia Akab: «Nimetumwa kukuletea maneno ya Rabbi. Kwani ukamwua Nabot, unyanganye shamba lake, mbwa waliolamba damu yake watakuja karibu kulamba damu yako. Yezabel nae atatafunwa na mbwa.»

III

Uaguzi huo ukatimia kweli. Miaka mitatu baada ya kuuawa Nabot, wafalme Yosafat na Akab wakapatana, wafuatane kuwashambulia maadui, waliowanyanganya mji wa Ramot katika nchi ya Galaad. Marra walipopambana na maadui, Akab akapigwa mshare garini mwake, akasinukia chini, akazimia roho. Mbwa wakaja wakalamba damu yake.

IV

Wânao Akab na Yosafat wakafanana na mfalme Akab, wakafuasa mifano yake, wakawa wabaya. Mwiny'ezi Mungu akawakasirikia akamwonya nabii Elise amteue mfalme mwingine, ndiye Yehu. Nabii akamwendea Yehu, akampaka mafuta matakatifu, akamweka mfalme.

Basi, kama miaka senashara nyuma ya kufa Akab, Yehu akamwua Yoram bin-Akab, akamwua Okosias bin-Yosafat, akaujitwalia ufalme. Siku alipokuja mjini Yezrael wakati wa kuingia akainua macho, akamwona Yezabel amesimama dirishani darini, ametia rangi machoni, amepamba kichwa chake. Yehu akawaamuru askari wamwangushe chini. Yezabel akatupwa, damu yake ikaruka ukutani; akakanyagwa na farasi, akazimia pale pale.

Mbwa wakaja, wakamtafuna mikono, na miguu, na kichwa.

V

Ndivyo ilivyotimizwa amri ya Mungu juu ya Akab, na juu ya Yezabel. Yehu akawaua wâna wote wa Akab, asisalie hatta mume mmoja wa ukoo wake; akaondoa ibada ya sanamu, ndiyo ibada ya Baal. Mambo yake yakampendeza Mungu, yakamwongokea.

43. MAFUMBO YA MFALME SELEMANI.

6. HAKI

18. Mizani iliyo na tafauti ina machukizo kwa Rabbi, ndiye mtaka mawe matimilifu. *Mafumbo, XI, 1.*

19. Mambo kwa huruma na haki humpendeza Mungu, kuliko sadaka. *Mafumbo, XXJ, 3.*

20. Bora kidogo kwa haki, kuliko mali nyingi kwa uovu. *Mafumbo, XVI, 8.*

7. HURUMA

21. Mwinyi huruma na haki humpendeza Rabbi, kuliko mwinyi kutoa sadaka. *Mafumbo, XXI, 3.*

22. Amwonaye huruma maskini, amkopesha Mungu, atalipwa. *Mafumbo, XIX, 17,*

23. Usimzuie mweza kumfanyizia mwenziwe; nawe, ukiweza, mfanyizie mwenz'ako. *Mafumbo, III, 27.*

24. Watu wachao Mungu si wabaya, wana huruma. *Mafumbo, XIII, 13.*

44. NABII ELISE.

I

Elise akatenda mâmbo mêngi sana: akafufua mtoto mmoja; mwaka wa ndjaa akawalisha watu wa Galgala kwa mikate ishirini; akamponya ukoma wake Naaman, jemadari wa mfalme wa Sham.

Naaman alikuja kutaka amwombee Mungu, amponye. Elise, aliposikia Naaman amekuja, mwenyewe asitoke kuonana nae, akampelekea mtu wake amwambie: «Enenda, ukoge marra saba maji ya Yordani, utatakata.» Naaman akafanya chuki, akanena· «Niliona angekuja kuniangalia na kunigusa ukoma wangu na kuniombea, kuniponya vile. Ya nini koga maji ya Yordani? Je! Hakuna kwetu mito yênyi maji mazuri zaidi? Akataka kwenda zake kabisa. Watumishi wake wakamtuliza, wakamwambia: «Bwana, kama nabii angalitaka jambo kubwa, ungalifanya hakika. Kama ametaka jambo dogo, akisema — Koga, utatakata —, afazali ushike maneno yake.» Naaman akashika shauri hiyo, akashuka mtoni, akaoga marra saba, akatakata kabisa. Akarejea, akamwamhia nabii: «Nimejua kweli hakuna Mungu ila Mungu wenu peke yake. Tokea leo sitoi sadaka mbele ya sanamu, nitamwabudu Rabbi. Tafazali upokee kitu cha mtumwa wako.»

Elise akaitika: «Kweli, sitaki kitu.» Akakataa, asipokee feza wala chochote.

II

Basi Naaman alipoondoka, mtumishi wa Elise, ndiye Giezi, akafanya ujandja apate kitu. Akamkimbilia Naaman nyuma, hatta alipompata akamwambia: «Nimetumwa na bwana wangu kukwambia: — Vijana wawili wamekuja sasa hivi, ndio wageni wangu, tafazali wape rupia alfeini.» Naaman akampa rupia arbat'alaf. Giezi akarejea zake, akaficha feza. Alipomwendelea bwana wake, akaulizwa: «Watoka wapi?» Giezi akaitika: «Sikwenda pahali.» Elise lakini alivumbua uongo wake: akakasirika, akamwambia: «Je! Akili yangu haikuwapo pale mtu alipogeuka nyuma, uliposhika feza yake? Basi ukoma wa Naaman utakuambata milele.» Toka siku ile Giezi akafanya ukoma, akaenea mabalanga.

Ndiyo hayo mâmbo Mwiny'ezi Mungu aliyomtendeza nabii wake, watu wapate kuamini maneno yake.

45. MAFUMBO YA MFALME SELEMANI.

25. Watu wengineo, wajapogawa mali zao na maskini, wapata zaidi; wengineo wajaponyânganya cha watu, wapungukiwa daima. *Mafumbo, XI, 24.*

26. Mziba sikio asimsikize maskini, akija nae kulalama, hapana wa kumsikiza. *Mafumbo, XXI, 13.*

27. Mtukana maskini, mtukana Muumbawe. *Mafumbo, XIV, 31.*

28. Mchukia bin-Adamu ana zambi; mwangalia maskini yatamwongokea. *Mafumbo, XIV, 21.*

29. Mzarao maskini amkosa heshima Muumbaye; nae, aliyefurahiwa akimwona mtu amepatikana na neno, hataepa azabu. *Mafumbo, XVII, 5.*

30. Usimtie nguvu maskini kwamba ni maskini, wala usimsonge mkiwa barzani kwa mashtaka. *Mafumbo, XXII, 22.*

31. Mtu mcha Mungu ajua nyama zake wana roho; watu wasio na dini wana moyo mgumu. *Mafumbo, XII, 10.*

8. UAMINIFU

32. Mdanganyifu ndiye atoaye siri za watu; mtu amini azuia maneno aliyoambiwa na mwenz'ake. *Mafumbo, XI, 13.*

33. Mawingu ya pepo makosa mvua, ndio mfano wake mjivunaji avunjaye maagano. *Mafumbo, XXV, 14.*

46. TOBI

I

Katika Waisrail waliochukuliwa Ninawi kulikuwa mtu mmoja mtakatifu sana, ndiye Tobi. Akampendeza mfalme Salmanasar, akapata heshima. Alipokufa Salmanasar, mwanae Senaharibu akawa mbaya kwa Tobi na kwa Waisrail wote, akawatesa, aka-

wanyanganya mali, akawaua wêngi, akikataa wasizikwe. Tobi hutoka usiku, huenda kuwaangalia nduguze, huwapa maskini chakula na nguo, huwazika mayiti. Siku moja, akêsha kuzika mayiti, akachoka, akalala ndjye: mavi ya kigumba-mshare yakamwangukia machoni, akaugua macho, akawa kipofu. Mbali kumtukana Mungu, akamshukuru kwa sababu ya mateso.

II

Mkewe Hanna huenda killa siku kufanya kazi kwa watu, apate chakula chake na cha mumewe. Kazi yake kufuma nguo. Siku moja akaja zake nyumbani na kibuzi, aliyempata zaidi ya mshahara wake. Tobi akamkataa kibuzi, akamwambia mkewe: «Labda kibuzi huyu ameibwa. Mwiko sisi kula au kupokea kitu kilichoibwa. Basi mrudishe, kampe mwenyewe.»

III

Tobi, alipokuwa mzee, akamwita mwanae Tobi mdogo, akampa mashauri mêma, akimwambia:

«Mwiny'ezi Mungu atakaponiita, ukêsha kunizika, usimwache mama wako. Mtukuze maisha yako, ukikumbuka usumbufu aliosumbuka sababu yako. Akifa nae, umzike pale pale nilipo.

«Mche Mungu siku zote. Usipokee zambi moyoni mwako. Hasa jiepuka na zambi ya uchafu. Ukatae majivuno: usijione mkubwa,

semee makubwa wala usiji; kwani majivuno huwa shina la zambi nyingi. Ukitaka shauri, utake kwa mtu aliyenyoka mbele ya Mungu.

« Mtu aliyefanya kazi kwako, mpe haki yake.

« Usiwatende watu mâmbo usiyopenda kutendewa mwenyewe.

«Wape maskini cha mali yako. Ukiwa na mali nyingi, wape zaidi; ukiwa na mali kidogo, wape kidogo kwa moyo mwema.

« Msifu Mungu daima, ukitaka kutenda mâmbo yaliyompendeza, ukikataa lolote alilokataza. Ukifanya hivyo, usiwe na woga. Tujapokuwa maskini, basi tukimcha Mungu, tukikataa zambi, tukitenda mêma, tutafanyiziwa mâmbo mêngi. »

Tobi mdogo akapokea moyoni mwake mashauri ya babae, akamwitikia: «Baba wangu, nitafanya chochote ulichonionya. »

IV

Tobi mkubwa akamtuma mwanae, aende mbali, katika mji wa Ragesi, kutaka feza aliyomkopesha Gabelus, rafiki yake. Tobi mdogo akatoka kutafutia kirongozi, akakutana na kijana aliyefunga safari. Akamwona uso wake mwema, mzuri mno. Nae kijana si bin-Adamu, ndiye malaika Rafail, aliyetumwa na Mwiny'ezi Mungu kumwongoza Tobi. Tobi mdogo akamwuliza kijana: «Rafiki yangu, wajua ndjia ya Ragesi?» Kijana akaitika: «Nimejua.» Tobi mdogo akapatana nae, akamleta nyumbani kwa baba. Kijana akamwamkia Tobi mkubwa, akamwambia: «Nitamwongoza mwanao mpaka Ragesi; kesha nitamleta.» Tobi mkubwa akanena: «Heri!

Safirini. Naomba Mungu amtume malaika wake kumpelekani.»

V

Basi Tobi mdogo akaondoka. Mbwa wake akamfuata. Siku ya kwanza wakafika mtoni Tigre. Tobi akashuka mtoni akoge miguu. Alipoingia majini, akaja samaki mkubwa akifunua mdomo kutaka kumwuma. Tobi akafanya woga, akapiga mayowe. Malaika akamwambia: «Mkamate kwa mashavu, kamvute ndjye.» Tobi akamkamata, akamleta juu. Malaika akamwambia: «Mpasue, mtoe matumbo, uweke moyo na maini na kibofu cha nyongo, kwani dawa.» Tobi akafanyiza vile. Kêsha wakaoka samaki: kipande wakala; chalichosalia wakatia chumvi, wakachukua, ndicho chakula cha njiani.

VI

Wakênda, wakênda hatta wakafika katika mji mmoja, wala sipo Ragesi bâdo. Malaika akamwambia: «Mjini hapa yupo mtu mmoja, jina lake Rageli, ukoo wako. Tuingie kwake. Ana mwanae Sara: basi mpose; babae hatakataa.» Tobi akaitika: «Nikasikia kama Sara amekwisha olewa na waume saba, nao wote saba wakafa arusini: Ni-

mesikia kama shetani aliwaua. Basi naogopa kunijia nami vile. Nami ni mwana wa peke: nikifa, baba na mama watasikitika mno, watakufa kwa uchungu.» Malaika akamwitikia: «Shetani hamwezi mtu, ila mwinyi zambi, kama watu wênyi kuoa kwa sababu ya tamaa mbaya, wakizarao Mungu. Walakini wewe sivyo. Ukêsha mwoa mwali, ushinde nae siku tatu mkisali mkiomba Mungu: ndivyo mtamtenga shetani.

VII

Basi wakaingia kwa Rageli. Rageli aliposikia mgeni wake ndiye Tobi, akamkumbatia, akamwambia: «Mungu akubariki mwan'angu. Baba wako namjua, mtu mwema sana, mwinyi fazila nyingi.» Akawaambia: «Karibuni, tule chakula.» Tobi akaitika: «Sili kitu kwako, kama hukunielekea kwanza kwa hayo nitakayo kwako; kwani nimekuja kumposa mwanao Sara.» Rageli, akiwaza mâmbo yaliyowapata watu saba waliokwisha kumposa Sara, akasita kwanza, asifunue kinywa. Malaika akamwambia: «Usiogope kumwoza mwanao kumpa kijana huyu, kwani mcha Mungu: nae ndiye mume aliyemtaka Mwiny'ezi Mungu kumpa mwanao. Ndiyo sababu wêngine wasimpate.» Rageli akaamini, akawaoza wâna, akaunga pamoja mkono wa kuume

wa mwanae na mkono wa kuume wa Tobi, akawasalia, akinena: «Naomba Mungu wa Ibrahimu, wa Izahak, wa Yakubu awaelekee hawa kuwaunga, kuwabariki.» Kêsha wakakaa kitako, wakala. Tobi na Sara wakashinda siku tatu kusali na kuomba, wasipatikane na baya lolote.

VIII

Tobi hakufika Ragesi. Malaika akamwacha kwa Rageli, akênda peke yake kumtakia feza yake kule; kêsha akarejea kitema nayo.

Kêsha siku hamstashara Rageli akamwambia Tobi: «Tafazali ushinde kwetu bâdo.» Tobi akanena: «Niachie niende zangu; kwani baba na mama huhasibu siku nitakaporudi; nikikosa, watafanya uchungu mno.» Rageli akamwachia, akampa nusu ya mali zake, akamsafirisha pamoja na mkewe Sara. Asijue kirongozi wao ndiye malaika, akawabariki, akinena: «Malaika wa Mungu ampelekani ndjiani, mpate kufika nyumbani salama.»

IX

Kwanza wasijefika, Malaika akamwambia Tobi mdogo: «Ukêsha ingia nyumbani, twaa nyongo za samaki, upake macho ya baba wako: ndiyo dawa yake; ataona mwangaza, atafurahi kukuangalia.»

X

Walakini baba na mama yake waliona siku nyingi, walisikitika sana. Mamae hutoka machozi, hulia, akinena: «Mwan'angu! Mwan'angu! Ya nini tukakutuma mbali huko? Wewe mwangaza wetu; wewe mkongojo wetu; wewe shime yetu; wewe matumaini yetu. Wewe ukiwapo, tuna ungi wa mali. Tukafanyiza vibaya tulipokutuma.» Mzee Tobi alitaka kumtuliza, akinena: «Tulia, usifanye uchungu kama huu. Mwana wetu mzima ati. Kirongozi tuliompa mtu amini.» Asipate lakini kumtuliza sana. Hanna ni kulia tu: siku zote huenenda ndjiani, hatta akifika kilimani, hukaa kitako, huangalia mbele, akiwaza mawazo ya uchungu. Siku moja akamtambua mwanae yule anakuja, akashuka upesi, akamletea habari mumewe, akimwambia: «Mwanao anakuja.» Marra mbwa, aliyefuatana na wasafiri, akaja mbio nyuma ya Hanna, akimshangilia bwana wake. Tobi mkubwa akajua kweli, akasimama, akashika mkono wa mtumishi wake, akatoka nae kumwendelea mwana, hatta akimkuta, akamkumbatia. Wakatoka machozi wazee kwa jinsi waliyofurahiwa. Tobi mdogo nae akafurahiwa, akiwaona baba na mama wazima.

XI

Wakashukuru Mungu. Kêsha Tobi mdogo akatwaa nyongo za samaki, akapaka macho ya babae. Yakatoka maganda mêupe, hatta ikêsha nusu saa, Tobi mzee akaona mwangaza, akapona. Akashukuru Mungu, akisema: «Nakusifu, Rabbi yangu, kwani uliponitesa ukaniponya. Sasa nimefurahiwa nikimwona Tobi mwan'angu.»

XII

Tobi mdogo akamsimulia baba mâmbo yote aliyotendewa na kirongozi wake, akanena: «Mêma yake mêngi, tusiweze kuyalipa. Basi naomba umtolee nusu ya mali niliyoleta.» Wakamwita kirongozi, wakataka kumtolea nusu ya mali. Akawaitikia: «Shukuruni Mungu, kwani ndiye aliyemfanyiziani. Kusali, kufunga, kuwapa maskini hupita mali yote. Ulipokuwa ukizika mayiti usiku, ukiomba Mungu, mimi humtolea Rabbi sala zako. Ukampendeza, ukaoneka amini: ndiyo maana ukajaribiwa. Leo Rabbi amenituma nikuponye. Ndimi Rafail, mmoja wa malaika saba wanaosimama mbele ya Mungu.» Wakisikia hayo, wakasangaa, wakaanza kutetemeka kwa woga, wakaanguka chini wakiinama uso. Malaika akawaambia: «Amani! Amani! Msiogope. Nili-

tumwa na Mungu kwenu. Mtukuzeni.» Basi, akafutika mbele zao, wasimwone têna.

Wakasifu Mungu, wakawasimulia watu mâmbo yaliyowapata. Tobi mkubwa na Tobi mdogo wakakaa siku nyingi, wênyi ungi na baraka ya Mungu.

47. NABII DANYEL SHIMONI KWA SIMBA.

I

Watu wa Babila waliabudu na chatu mkubwa. Siku moja mfalme akamwambia Danyel: «Abudu mungu wangu. Huwezi kunena — si mzima. —» Danyel akaitika: »Naabudu Mungu wangu, ndiye aliye mzima kweli. Huyo wako siye mungu mzima kweli. Ukinipa ruhusa, nitamwua, hakuna kwa upanga, hakuna kwa ufito.» Mfalme akampa ruhusa. Danyel akatwaa lami na mafuta na manyoya ya nyama, akachanganya pamoja, akafanya madonge, akayatupa mdomoni mwa chatu. Chatu akameza. Asiweze kuvumilia chakula kizito hicho, akawa hawezi, akafa. Ikaonekana si mungu: kwani Mungu haogopi sumu wala chakula kibaya. Danyel akamwambia mfalme: «Ndiye huyu mungu wako uliyemwabudu!»

II

Mfalme akanyamaa. Watu wa mji lakini wakachaga, wakamchongea Danyel jinsi yote kwa mfalme, wakataka atupwe shimoni kwa simba. Mfalme alimpenda Danyel, wala hakusadiki uchongezi wa watu, akamwonea huruma. Mwisho lakini akaogopa watamwua mwenyewe, akawaachia ruhusa wamtupe Danyel shimoni kwa simba. Shimoni mle walikuwamo simba saba, wakali mno, wasiotolewa chakula siku ile. Basi Danyel alipotupwa shimoni, hawakumwumiza hatta, ila wakamnyenyekea. Siku ya saba toka alimo shimoni, Danyel akaona ndjaa, akaomba Mungu.

III

Basi siku ile ile palikuwa nabii, ndiye Habakuk, aliyekaa kwenye mahame ya Yerusalem, mwendo wa mwezi mzima. Alikipika chakula chake, malaika akamtokea, akamwambia: «Chakula ulichopika mpelekee Danyel, aliyefungwa shimoni kwa simba katika mji wa Babila.» Habakuk akaitika: «Sijaona Babila; sijui shimo wapi.» Basi malaika akamshika utosini kwa nywele zake, akamchukua juu, akampeleka kwa marra moja hatta Babila kando ya shimo la simba. Habakuk akamwita

Danyel mle, akanena: «Mtu wa Mungu, pokea chakula alichokuletea Mungu.» Danyel akaitika: «Ee Mungu wangu! Ukanikumbukia. Huwaachi wapenzi wako.» Akasimama, akala chakula. Malaika akamtwaa Habakuk, akamrudisha kwake.

IV

Siku ya saba mfalme akaja kumlilia rafiki yake. Akaangalia shimoni, akamwona yu mzima kati ya simba. Akasangaa, akasema: «Ee! Rabbi wa Danyel, ndiwe Mungu mkuu.» Akamtoa Danyel, akatoa amri watu, waliomchongea, watiwe shimoni. Simba wakawatafuna marra. Mfalme akasema: «Watu wote wamche Mungu wa Danyel; kwani ndiye mwokozi, mwinyi kutenda miujiza; ndiye aliyemwokoa Danyel katika shimo la simba.»

48. MAFUMBO YA MFALME SELEMANI.

9. MAJIVUNO, UNYENYEKEO

34. **Majivuno, mbeleye maangamizi: mwinyi kujisifu amekwisha ngia ndjia ya upotevu.** *Mafumbo XVI, 18.*

35. **Majivuno, mbeleye upotevu: ajikuzaye leo, kesho atakwaa.** *Mafumbo, XVI, 18.*

36. **Ajivunaye, mwishowe atapatikana na haya; ila mnyenyekevu atatukuzwa.** *Mafumbo, XXIX, 23.*

37. Bora maskini mwenda kwa unyofu, kama mwinyi mali mpotoa mdomo, au kama mfanya wazimu. *Mafumbo, XIX, 1.*

38. Sijione mtu wa hekima: mcha Mungu, epa uovu. *Mafumbo, III, 7.*

10. UPOLE

39. Majibu kwa upole humpoza mwinyi hasira; maneno magumu huwasha. *Mafumbo, XV, 1.*

11. UGOMVI

40. Bora donge la mkate kwa furaha, kama vyakula tele nyumbani pamoja na ugomvi. *Mafumbo, XVII, 1.*

41. Pakosapo kuni, moto wazimika; paondokapo mtu mpetekefu, ugomvi wakoma. *Mafumbo, XXVI, 20.*

12. MABEMBELEZI

42. Bora kugombezwa na mtu wa hekima, kama kudanganywa na mabembelezi ya wapumbavu. *Mashauri, VII, 6.*

13. ULIMI

43. Mzuia midomo yake atunza roho yake; mpesi wa kunena ataondja mabaya. *Mafumbo, XIII, 3.*

44. Panapo maneno mengi, haikosekani zambi; mzuia midomo yake, utartibu wake si mchache. *Mafumbo, X, 19.*

45. Maneno ya msema kwa tartibu yapendeza, kama machungwa katika sahani ya feza. *Mafumbo XXV, 11.*

46. Ulimi mtoa uongo hauvumiliwi: una machukizo kwa Rabbi. *Mafumbo, XII. 22.*

47. Ulimi mtoa uongo wamwua mwenyewe. *Hekima, I, 11.*

48. Mchongea uongo nyuma, na nyoka aumaye na kimya, uovu mmoja. *Mashauri X, 11.*

49. Simsogeze mwinyi ulimi mwovu; waambaji sandamane nao. *Mafumbo, IV, 24.*

50. Asikizaye ulimi mwovu ni mwovu; mvumilia uongo ni mwongo. *Mafumbo, XVII, 4.*

51. Moto karibu na makaa na kuni, na mgomvi mpekecha watu, mambo mamoja.

49. NDUGU SABA AKINA MAKABE. MASHAHIDI WA DINI.

I

Siku moja, mfalme Antiokus akamkamata mama moja na wanawe saba, jina lao Makabe. Akawaambia waache dini, wasifuase sharia ya Mungu. Wakakataa. Akafanya hasira, akawakonyeza askari wawatese ndugu hawa wakaidi. Watoto wakipigwa mabakora, wakakaa imara, hatta mkubwa akanena: «Watutakia nini? Tu tayari kufa, ila tusivundje sharia ya Mungu.» Antiokus akawaka, akaamuru akatwe ulimi, miguu na mikono, achunwe ngozi ya kichwa, atiwe katika sufuria ya moto. Askari wakamtenda vile walivyoamriwa, mwenyewe asiregee hatta, mamae na nduguze wakimtia moyo, wakimwambia — vumilia —. Alipokwisha wa kwanza, akasumbuliwa wa pili. Akizimia huyo, aka-

mwambia mfalme: «Leo watuua; kesho Mfalme wa ulimwengu atatupa uzima wa milele; kwani tunakufa mashabidi ya amri zake.» Akitakwa wa tatu, akachekelea, mwenyewe akatoa mikono, akatoa na ulimi akatwe, akinena: «Mapaji haya nikayapokea kwa Mungu; leo nayatoa, nisipate kuvundja amri zake: Mwenyewe ataniponya.» Basi wa nne, na wa tanu, na wa sita, wakateswa vile vile, wakavumilia wasiregee kabisa.

II

Mwisho walisalia mwana-mdogo na mamae. Mfalme akambembeleza mwana, akamwambia atampa mali, atampa chochote, atamfanya rafiki yake, mwenyewe akikubali kuacha dini. Akimwona mkaidi kama nduguze, akamwambia mama ampe mwanae shauri jema, amwokoe. Mama akamjongea mwana, akamwambia: «Mwana, kipendi changu, nakuambia uangalie uwingu na nchi na viumbe vilivyomo, ukumbuke ndiye Mungu aliyeumba hayo yote. Kwani usimwogope muuaji huyu. Uwe na moyo mkuu kama nduguzo, ufanane nao, nipate kukuona pamoja nao uwinguni milele.» Mwana mdogo hakusita hatta kidogo. Mamae asijêsha kusema, akanena: «Mwangojani? Sishiki amri ya mfalme,

ila nashika amri ya Mungu. Wewe, mfalme, uliyetenda maovu kwetu, hutaepuka na hasira ya Mungu.» Mfalme akafanya uazimu kwa jinsi alivyowaka, akaamuru mwana mdogo ateswe zaidi ya nduguze. Akafa basi; mamae akauawa nae mwisho.

50. MAFUMBO YA MFALME SELEMANI

14. TAKATO

52. Mawazo mabaya yana machukizo kwa Rabbi. *Mafumbo, XV, 26.*

53. Awezaje mtu kufutika kijinga cha moto nguoni mwake, asiwake. Au awezaje kukanyaga makaa ya moto, asiungue nyayo zake? *Mafumbo, VI, 27-28.*

54. Mzinifu ajikusanyia haya na machukio kichwani mwake: kilema chake hakitaondoka. *Mafumbo, VI, 32-33.*

55. Epuka na cherevu cha mwana-mke: mdomo wa kahaba tamu kama asali ya nyuki, na kinywa chake cha ulaini kuliko mafuta; kinyume chake ni uchungu wa pakanga, kina makali ya upanga wa feleji; ndjia yake ya Motoni. *Mafumbo V, 2-5.*

56. Mapendezi huwa na udanganyifu, uzuri si kitu; ila mke mcha Mungu, ndiye mwinyi kusifiwa. *Mafumbo, XXXI, 30.*

15. URAFIKI MBAYA

57. Mwenda na watu wenyi hekima atapata hekima; mwenda na wenyi wazimu hana budi kufanana nao. *Mafumbo, XIII, 20.*

58. Rafiki mbaya amvutia rafiki yake: ampelekeapo si pazuri. *Mafumbo, XVI, 29.*

59. Mwan'angu, wazambi wakitaka kukuvutia, usiwasikize. Wakinena Ndjyoo nasi, usifuatane nao; kwani mwendo wao na mbio yao kwa mabaya: shika mfano wa ndege aliyetambua mtego, akarukia mbali. *Mafumbo, I, 10, etc.*

60. Mwenda na mtu mtakatifu, mfano wake ni mwanga wa jua: wakua na jua kupanda. Mwendo na watu wabaya una jiza: huenda, wasijue ukomo wao ni kupotea. *Mafumbo, IV, 18.*

16. NDJIA YA WATU WABAYA

61. Iko ndjia moja ionekanayo barabara: ukiishika, ukomo wake ni kufa. Ndiyo ndjia ya zambi. *Mafumbo, XV, 25.*

17. ADUI

62. Bora rafiki muumiza ampendaye, kama adui mdanganyifu akimbusu yule amwoneaye. *Mashauri, VII, 6.*

63. Adui mwinyi ndjaa mpe chakula; akiwa na kiu, mpe maji: yatakuwa kama makaa ya moto katika kichwa chake, na wewe Mungu atakurudishia. *Mafumbo, XXV, 21-22.*

51. MWANA WA JUMBE

Siku moja Yesu akênda zake Kafarnaum. Palikuwa na akida mmoja, Mroma, mtu mwema, na mtu wake hawezi sana. Basi akida yule akisikia Yesu amekuja mjini, akatuma watu wamwite aje kumponya mtu wake. Yesu akafuatana nao, hatta alipofika karibu na nyumba, yule akida akamtokea mbele, akamwambia: «Rabbi, mimi mtu gani uingie kwangu! Useme neno moja tu, mtu wangu apone.

Ndivyo kama mimi, mtu wa sirkali, nina askari chini yangu: nikimwambia huyu — Nenda —, huenenda, na mwingine — ndjyoo —, huja, na mtumwa wangu — fanya hii — hufanya.» Yesu akisikia maneno yake, akasangaa, akawaambia waliomfuata: «Namwambiani kweli, sikuona katika Waisrail mtu wa imani kama huyu. Namwambiani basi kama wêngi watatoka Mashariki na Mangaribi, nao watapata kikao katika ufalme wa mbinguni pamoja na Ibrahimu, na Izahak, na Yakub. Wana wa ufalme lakini watatupiliwa mbali dyizani: ndiko kwenye kulia na kutafuna mêno.» Basi Yesu akamwambia akida: «Nenda, upate hayo uliyoaminia.» Mtu wake akapona saa hiyo hiyo.

Watu wa Mashariki na wa Mangaribi watakaopata kikao uwinguni, ndio Washenzi watakaokubaliwa na Mungu. Kwani Mayahudi wêngi wakamkataa Yesu, wakapotea. Nao wageni wêngi wakaamini, wakabatizwa, wakawa watoto wa Mungu.

52. MAFUNDISHO YA YESU KRISTU.

1. HERI YA KWELI

«Heri yao wasio na tamaa; kwani watapata kuingia katika ufalme wa mbingu.

Heri watu wênyi upole; kwani watapata kuingia katika Nchi ya Dyuu.

Heri wênyi kulia; kwani watatulizwa.

Heri wênyi ndjaa na kiu; ndiyo kwa kutaka utakatifu; kwani watashiba.

Heri wênyi huruma; kwani nao watapata huruma.

Heri wênyi moyo safi; kwani watamwona Mungu.

Heri wênyi kutaka amani; kwani wataitwa watoto wa Mungu.

Heri wanaosumbuliwa kwa sababu ya mâmbo mêma; kwani wataingia katika ufalme wa mbingu. Heri nyinyi, mkiapizwa na watu, mkisumbuliwa nao, mkichongewa urongo kwa ajili yangu mimi: muwe na furaha kuu; kwani tuzo lenu litazidi mbinguni.»

2. SALA.

«Mnaposali, msifanye kama wanafiki, wapendao kusali wakisimama katika masunagogi na katika panda ya ndjia, waonekane na watu. Wewe, unaposali, ingia chumbani kwako, funga mlango, mtolee Baba wako sala zako za ndani; naye Baba wako, aonaye ya ndani atakurudishia.»

Mkisali msitoe maneno mêngi kama washenzi: kwani watu hao huzani watasikilizwa, maneno yao yakiwa mêngi. Msifanane nao, kwani Baba wenu ajua mwatakayo, hatta kwanza msijapoomba,

Basi mtakaposali, şalini hivi:

Baba 'etu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe,

ufalme wako utufikie, utakalo lifanyike katika nchi kama uwinguni. Utuletee leo mkate wetu wa killa siku, utuondolee makosa yetu kama twawaondolea waliotukosa, wala usitutie katika kishaushi, walakini utuopoe maovuni.

Ombeni, mtapewa; tafuteni, mtapata; pigeni hodi, mtafunguliwa. Kwani yeyote aombaye, hupewa; na atafutaye, hupata; na apigaye hodi, hufunguliwa. Au yupi mtu kwenu, mwanae akiomba mkate, basi ampe jiwe? Au akimwomba samaki, atamtolea nyoka? Basi kama nyinyi, mlio waovu, mwajua kuwapa watoto wenu mêma, kama nini zaidi Baba wenu, aliye mbinguni, atawapa mêma wamwombao?»

53. WATU ALFU TANU WANALISHWA UWANDJANI.

I

Siku kidogo mbele ya siku-kuu ya Paska, Mitume wakamrejea Yesu, wakampasha habari ya mâmbo waliyoyatenda. Yesu akawaambia: «Twendeni uwandjani tukapumzike kidogo. Wakaingia nae chomboni, wakavuka bahari ya Galile, wakaja zao ńambo ya pili, wakaingia uwandjani: Watu wêngi lakini waliwafuata. Wakamfuata mbali kwa

tamaa ya kumsikiliza, nao katika haraka yao hawakuwaza wachukue vyakula pamoja nao. Basi Yesu akawahurumia, akiwaona wanamfuata wasipumzike wala wasirejee nyuma. Akakaa kitako, akamwuliza Filippi: «Mikate tununue wapi, wapate kula watu hawa?» Mwenyewe alijua atafanyaje. Filippi akamwitikia: «Mikate ya vipande miateini vya feza haiwatoshi, kulla mtu apate kidogo!» Andre akamwambia: «Yupo kijana: ana mikate mitanu na samaki mbili. Hufaa nini lakini kwa watu wêngi hawa?» Basi Yesu akasema: «Waambieni watu wakae kitako.»

II

Palikuwa na majani mêngi huko. Basi watu wakakaa kitako, wapata kama alfu tanu. Yesu akapokea mikate, akashukuru Mungu, akawagawanyia, akawapa na samaki kadiri watakayo. Walipokwisha shiba, akawaambia wafuasi wake: «Kusanyeni makombo yaliyosalia, yasipotee.» Wakakusanya, wakajaza vikapo ṣenashara. Watu wale, walipoona muujiza aliotenda Yesu, wakanena: «Huyu kweli ndiye Nabii, tuliyemsikia atakuja duniani.» Basi Yesu akiona watu wataka kumwungama mfalme wao, akawaambia wafuasi wake wapakie chomboni, wa-

vuke kwenda Bet-saida. Mwenyewe akaondoka kwa siri peke yake, hatta usiku akifika mlimani, akakaa akisali kutwa.

54. MAFUNDISHO YA YESU KRISTU.

3. KUFUNGA

«Mnapofunga, msijikunate uso kama wanafiki: kwani hugeuza nyuso zao, waonekane na watu wanafunga. Wewe, wafungapo, nawa uso, paka kichwa kwa mafuta, usionekane na watu unafunga, uonekane tu basi na Baba wako ajuaye ya ndani; naye, Baba wako ajuaye ya ndani, atakutuza.»

4. MALI SI KITU

«Msijiwekee mali duniani, kwenyi funza na kutu hula, kwenyi na wêvi huchimba huiba. Walakini jiwekeeni mali uwinguni, kusiko wala funza wala kutu kutafuna, kusiko wala wêvi kuchimba na kuiba. Kwani pale ilipo mali yako, upo na moyo wako. — Mtu mmoja hawezi kutumika kwa bwana wawili. Hamwezi kutumika kwa Mungu na kwa feza. Kwani namwambiani: msiwazewaze mtapataje chakula msife, na nguo mvae kufunikia mwili... Angalieni ndege za anga: hawapandi, wala hawavuni, wala hawaweki uchagani: ndiye Baba wenu wa mbinguni mwinyi anawalisha. Je! Nyinyi si kuwa-

pita sana?.. Angalieni maua ya shamba yanavyoota: hayatendi kazi, hayasokoti uzi. Namwambiani basi kwamba Selemani mwenyewe, japo akawa na utukufu mwingi, hakupata kuvaa vizuri vile, kama ua moja lile. Kama Mungu basi huvika vile jani la shamba, twaloona leo, litakalochomwa motoni kesho, kama nini zaidi atamfanyiziani nyinyi, watu wa imani chache! Haya basi! Msisumbuke, mkinena: Tutakula nini, au tutakunywa nini, au tutavaa nini? Washenzi kweli husumbuka kwa hayo; mbali nyinyi. Kwani Baba wenu amejua mwataka hayo yote. Basi takeni kwanza ufalme wa Mungu na utakatifu wake, mtapewa na mêngine pia ziada.»

55. TAJIRI NA LAZAR.

I

Yesu akawaambia wafuasi wake mfano mwingine: «Palikuwa na tajiri, aliyevaa nguo nyekundu za kitani, akila karamu siku zote. Palikuwa na maskini, jina lake Lazər, aliyekaa kitako mlangoni kwa tajiri: ana madonda, ana ndjaa, wala hapati kushiba, akitamani makombo yaangukayo mezani kwa tajiri; nae tajiri hakumpa. Mbwa huja, hulamba madonda yake yule maskini. Basi mwisho

maskini akafa, akachukuliwa na malaika uwinguni, akae pamoja na Ibrahimu. Tajiri nae akafa, akashuka motoni.

II

Basi tajiri, akisumbua motoni, akiinua macho juu, akamwona Lazar anafurahi pamoja na Ibrahimu; akalia, akanena: — Baba Ibrahimu, unihurumie, unipelekee Lazar, achovye kidole chake majini, anipe nifyonze, nikate kiu kidogo, kwani naugua mno motoni humu. — Ibrahimu akamwitikia: — Mwan 'angu, kumbuka ukapata mêma duniani, nae Lazar akapata mabaya. Basi leo haki yake atulizwe, ila wewe haki yako usumbuke. Na kati yenu nasi mna shimo kuu, watu wa kwetu, wakitaka kupita kwenda kwenu, wasiweze; wala wa kwenu, wakitaka kuja kwetu, wasiweze. — Tajiri akanena: — Baba 'angu, nakuomba umpeleke Lazar nyumbani kwa baba 'angu, wakaapo ndugu zangu watanu, awaeleze habari za motoni, wasije nao kusumbuka humu. — Ibrahimu akamwitikia: — Wana Musa na Manabii: basi wawasikize. — Tajiri akanena: — Baba 'angu Ibrahimu, naona hawatawasikiza. Ila mmojawapo akitoka katika wafu, akiwaendea, watatubu. Ibrahimu akamwitikia: «Kwa-

mba hawasikizi wala Musa wala Manabii, hawatamsikiza hatta mtu aliyetoka kaburini, aliyefufuka.»

56. MAFUNDISHO YA YESU KRISTU.

5. MAMBO MÊMA.

«Mkitenda mâmbo mêma, angalieni msiyafanye mbele za watu, kusudi mwonekane nao: kwani mkitenda hivyo, hamtatuzwa na Baba wenu aliye mbinguni. Basi mnapotoa sadaka, msipige tarumbeta mbele yenu, kama wafanyavyo wanafiki katika masunagogi na ndjiani, wapate heshima kwa watu... Wewe ukitoa sadaka, hatta mkono wako wa kushoto usijue mkono wa kuume wafanyalo. Basi sadaka yako itoe kwa siri, naye Baba wako, aonaye siri, atakurudishia.»

6. UZANI.

«Msiwazani watu, wala nyinyi hamtazaniwa; msiwapatilize, wala nyinyi hamtapatilizwa. Waondoleeni, nanyi mtaondolewa... Kipimo mlichowapimia watu, ndicho mtakachopimiwa. — Mbona unaona ukumvi katika jicho la nduguyo, mwenyewe usione banzi zima jichoni mwako? Mnafiki, toa kwanza banzi la jichoni mwako, ndipo uwaze kutoa ukumvi jichoni mwa nduguyo... Mtakalo lolote kufanyiziwa na watu, nanyi imempasani muwafanyizie vile.»

7. URONGO.

«Umesikia wazee waliambiwa: Usiape urongo, ila umtimizie Mungu viapo vyako. Nami namwambiani: Usiape kabisa, wala kwa kutaja uwingu, kwani ndicho kiti cha Mungu; wala kwa kutaja nchi, kwani ndipo pa kutegemezea miguu yake; wala kwa kutaja Yerusalem, kwani ndio mji wa Mfalme Mkuu; wala kwa kutaja kichwa chako, kwani hatta unywele mmoja huwezi kuufanya wala mweupe wala mweusi. Maneno yenu yawe tu ndiyo ndiyo, siyo siyo; kwani la kuzidi hayo ndilo la uovu.

8. NDJIA NGEMA. UOKOVU.

«Ingieni kwa mlango mwembamba: kwani ndjia ya upotevu mpana, mlango wake una nafasi, na waingiao wêngi. Walakini ndjia ipelekayo kwenyi uzima, siyo pana, na mlango wake ndio wa kufinyana, wasiwe wêngi wênyi kuupitia... Angalieni msidanganywe na manabii wa uongo, wanaokuja kwenu wakivaa manyoya ya kondoo, nao kwa ndani ndio mbwa-mwitu wakali. Mtawatambua kwa matunda yao. Je! Huchuma wapi zabibu michongomani, na tini katika mbigili? Kwani ndiyo kulla mti mwema huzaa matunda mêma, na mti mbaya huzaa mabaya. Mti mwema haufay kuzaa matunda

mabaya, wala mti mbaya hauzai mêma. Kulla mti, usiozaa matunda mêma, utakatwa, utatupwa motoni. Basi ndivyo kwa matunda yao mtakavyowatambua. Kwani siye yeyote anayenambia — Rabbi! Rabbi! — atakayeingia katika ufalme wa mbingu, ila ndiye, ashikaye mapenzi ya Baba wangu wa mbinguni, atakayeingia katika ufalme wa mbingu... Killa mwinyi asikiaye maneno hayo, akiyashika, amefanana na mtu mwinyi akili aliyejenga nyumba yake katika nchi ya mawe. Naye mwinyi asikiaye maneno hayo, asiyashike, amefanana na mtu mpumbavu aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga: mvua ikanya, maji ya mito yakajaa yakatawanyika, pepo zikavuma, zikapiga nyumba ile, zikaliangusha: hasara yake ikawa kubwa.»

57. UFUFUO WA LAZAR.

I

Katika wafuasi wake Yesu alimpenda sana mmoja, jina lake Lazar, kwani mtakatifu sana. Lazar alikaa Betani karibu na Yerusalem pamoja na maumbu wake wawili Marta na Maryamu.

Siku moja, Yesu akisafiri katika Galile, Lazar akashikwa na ugondjwa mkali mjini kwake. Maumbu wake wakamtuma mtu mmoja kwenda ku-

mwambia Yesu. Mtu yule, alipokwisha mweleza Yesu, akarudi, akawaletea majibu ya Yesu wasiogope: «Ugondjwa huu si wa kufa, ila utafaa kuonya utukufu wa Mungu, Mwana-Adamu apate sifa.» Basi Yesu akazunguka bâdo siku mbili, akiwafundisha watu wa Galile, hatta siku ya tatu akawaambia wafuasi wake: «Twendeni zetu Betani. Lazar, rafiki yetu, amelala: ninakwenda kumwamsha.» Wafuasi wakamwambia: «Rabbi, kama Lazar amesinzia, atapona.» Kwani walizani Yesu amenena kulala usingizi.» Basi Yesu akawaambia wazi: «Lazar amekufa. Kwa sababu yenu ninafurahi kama sikuwapo, mpate kusadiki. Basi twende kwake.»

II

Yesu alipofika Betani, Lazar amekwisha zikwa toka siku nne. Maumbu wake wako ndani nyumbani wakilia, na marafiki yao wamekuja kuwatuliza. Basi Marta, aliposikia kwamba Yesu amekwisha fika, akamwendea, akamwambia: «Rabbi, kwamba ungalikuwapo hapa, ndugu yetu hangalikufa. Najua basi utakalo lolote kwa Mungu, atakupa.» Yesu akamwambia: «Ndugu yako atafufuka.» Marta akanena: «Kweli, najua atafufuka mwisho siku ya ufufuko wa watu wote. Yesu akamwambia:

«Ndimi mwinyi kufufua, na mwinyi kupa uzima. Anisadikiye, japo amekufa, atakuwa mzima; na killa aliye mzima anisadikiye, hatakufa milele. Je wasadiki hayo?» Akamwitikia: Ndiyo, Rabbi, ninasadiki kwamba ndiwe Masiha, Mwana wa Mungu mzima, uliyekuja duniani.»

III

Marta basi akaingia nyumbani, akamwita umbu lake Maryamu, ndiye Madelene, akamwambia: «Rabbi yuko, amekuja, anakwita.» Maryamu akasimama marra, akamwendea Yesu. Marafiki yake wakimwona anaondoka, wakaneneana: «Anakwenda zake kaburini kwa maombolezo», wakafuatana nae. Maryamu, alipomwona Yesu, akamwangukia, akilia, akinena: «Rabbi, kwamba ungalikuwapo, ndugu yangu hangalikufa.» Nao Mayahudi marafiki yake hulia, hutoka machozi pamoja naye. Yesu akiona sikitiko lao, akashituka moyoni mwake, akanena: «Mmemzika wapi?» Wakamwambia: «Ndjyoo, Rabbi, ukaone.» Akatoka machozi, hatta Mayahudi wakanena: «Angalieni, alimpenda sana kweli.»

IV

Pênye kaburi palikuwa pangoni, palifungwa na jiwe. Yesu alipofika, akanena: «Ondoeni jiwe.»

Marta akamwambia: «Rabbi, ananuka; kwani siku ya nne toka amezikwa.» Yesu akamwitikia: «Siku-kwambia ukisadiki utaona utukufu wa Mungu?» Wakaondoa jiwe. Yesu akainua macho juu, akinena: «Baba 'angu, ninakushukuru kwani umenisikiliza. Nilijua mimi wanisikiliza siku zote; illakini nikanena hayo kwa sababu ya watu wêngi hawa, wapate kusadiki ndiwe uliyenipeleka.» Akêsha kusema hayo, akapaliza sauti, akanena: «Lazar, toka!» Marra ile yule aliyekufa akatoka kaburini mwinyi miguu na mikono yametatiana vitambaa na kichwa kimefunikwa na sanda. Yesu akawaambia watu: «Mfungulieni, mwacheni atoke.»

58. MAFUNDISHO YA YESU KRISTU.

MFANO WA MBEGU.

«Mpanzi akatoka kusia mbegu. Basi anaposia mbegu, nyingine zikaanguka ndjiani, zikakanyagwa, zikaliwa na ndege za anga. Nyingine zikaanguka maweni, zikêsha mea zikakauka kwa kukosa maji. Nyingine zikaanguka katika miba, miba ikaota pamoja, ikazisonga. Nyingine zikaanguka katika nchi ngema, zikaota, zikazaa moja kwa mia.»

Akawafafanulia wafuasi wake maana: «Mbegu huwa neno la Mungu. Mbegu zilizoanguka ndjiani,

huwa watu ambao wanasikia; kêsha huja shetani, huondoa hilo neno moyoni mwao, wasipate kusadiki, wasiokoke. Nazo mbegu zilizoanguka maweni, huwa watu ambao, wakisikia neno, wanalishika kwa furaha, lakini hawana mizizi: huamini kipindi kidogo, hatta pindi la kujaribiwa hugeuka. Nazo mbegu zilizoanguka katika miba, huwa watu waliosikia, kêsha wakaenenda, wakasongwa na shuruli na mali na anasa za ulimwenguni, wasizae. Nazo mbegu zilizoanguka katika nchi ngema, huwa watu waliosikia neno kwa moyo mwema, wakalishika, wakavumilia, wakazaa.»

MFANO WA NGANO PAMOJA NA NDAGO.

«Ufalme wa mbingu umefanana na mtu aliyepanda ngano kondeni mwake. Walakini, watu wakiwa wamelala, adui yake akaja akapanda ndago katika ngano; kêsha akênda zake. Basi ngano ilipofanya majani kuota na kuzaa, zikaonekana na ndago. Wakulima wa bwana wakaja, wakamwambia: — Je, bwana, hukupanda mbegu ngema kondeni mwako? Mbona ndago imo? — Akawaambia: — Kazi hiyo ya mtu adui. — Wakulima wake wakamwambia: — Wataka twende tukañoe? — Akanena: — Siyo. Mkiñoa ndago mtaweza ku-

ñoa na ngano pamoja. Acheni mbegu mbili kukua mpaka mavuno. Siku ya mavuno ntawaambia wênyi kuvuna: — Kusanyeni kwanza ndago mkifunga machopa ya kuchomea moto. Ngano basi iwekeni ralani kwangu. — «Yesu akawafumbulia maana yake mfano huo. «Mwinyi kupanda mbegu ngema, ndiye Mwana-Adamu; konde ndiyo dunia; mbegu ngema ndio wâna wa Mungu; ndago ndio wâna wa shetani; adui aliyepanda ndago ndiye shetani; mavuno ndipo mwisho wa dunia; nao wênyi kuvuna ndio malaika. Basi kama vile ndago na mabiwi yanakusanywa, yanachomwa moto, vile vile, mwisho wa dunia, Mwana-Adamu atapeleka malaika wake, nao wataondoa katika ufalme wake watu wote wabaya, watawatupa motoni, ndiko kweni vilio na kutafuna mêno. Na hapo watu watakatifu watañara kama jua katika ufalme wa Baba wao mbinguni.»

SEHEMU YA TANU.

59. MWAKA, MWEZI, JUMA, SIKU.

Katika mwaka moja wa kizungu kuna miezi kumi na miwili, au juma hamsini na mbili, au siku mia tatu, sittini na tanu.

Killa mwezi una jina lake na siku zake: Yanuari (siku 31), Februari (28 au 29), Marsi (31), Aprili (30), May (31), Yuni (30), Yuli (31), Augusti (31), Septembri (30), Oktobri (31), Novembri (30), Desembri (31). Tunaona, mwezi wa kwanza una siku 31, wa pili una siku 30 tu; hatta mwezi Februari una siku 28 tu, na killa mwaka wa nne una siku 29.

Siku saba zafanya juma moja. Ndizo: Juma 'a pili (siku hiyo ya mwanzo), juma 'a tatu, juma 'a nne, juma 'a tanu, alhamisi, ijuma, juma 'a mosi.

Basi juma 'a pili, ndiyo siku ya Mungu, tuliyoamriwa tuache kazi, tusali.

Katika siku moja kuna saa ishrini na nne.

Katika saa moja kuna dakika sitini.

60. NCHI, JUA, MWEZI, NYOTA.

Nchi ni kubwa. Inazo bahari, na mito, na viziwa vya maji, na chemchem; inazo bara na visiwa, na vilima, na mabonde, na mashamba, na mapori, na nyika, na misitu, na majangwa.

Walakini jua ni kubwa zaidi kuliko nchi. Linaonekana ndogo, kwa maana li mbali mno.

Hatta mwezi ukiuangalia, utaona kwake penyi peupe na penyi peusi. Basi bara kubwa hiyo: penyi peupe ni mapori, penyi peusi ndipo milima.

Hatta nyota unazoona ndogo; basi si ndogo. Zinaonekana hivi kwa kuwa mbali. Kivimba chao sawa sawa na jua, na zaidi.

61. NCHI, JUA, MWEZI, PANDE ZA MAJIRA.

Nchi imeviringana kama chungwa. Nchi imekaa ulimwenguni isipokalia kitu: hukaa uwazi, ni vile vile kama jua lenyewe, na mwezi, na nyota.

— Nchi inapewa kwa jua mwangaza na moto.

— Tumesema: nchi inakaa. Walakini, nchi haikai pahali, inakwenda tu. Inalizunguka jua kulla mwaka duru moja. Jua linaonekana kama linakwenda: basi lenyewe linakaa, nasi tunakwenda.

— Hatta nchi yenyewe inapinduka kwa muda ya siku moja, na killa siku vile.

— Basi, nchi inapoelekea jua, kunapambauka: ndipo mchana. Nchi inapogeuka na jua, kunakuwa jiza: ndipo usiku. Mchana una vipindi vitatu: asubuhi, azuhuri na jioni.

— Basi, mwezi pia unazunguka nchi katika siku ishrini na saba, na saa saba, na dakika arbaini na tatu. Unapewa nae mwangaza wake kwa jua.

— Pande za majira ziko nne: **Kaskazi** ao jaha, **Kusini** ao junubi, **Mashariki** na **Mangaribi.**

— Mashariki ni upande jua linapotoka asubuhi. Mangaribi ni upande jua linapokuchwa jioni. Basi, ukitezama masharikini, mangaribi inakuwa nyuma, kaskazi inakuwa mkona wa kushoto, na kusini inakuwa mkono wa kuume.

62. SEHEMU ZA NCHI.

Nchi inazo sehemu tanu. Ndizo hizo: Ulaya, Asia, Afrika, Merikani, Australia.

Ulaya ni nchi ya Wazungu: Wadachi, Wafransa, Wangreza, Waaustria, Warusi, Warenu, Wagreki, Spenyol, Matalyani, Maturki, Mabelji, na wengine.

Asia ni nchi ya: Wahindi, Waarabu, Magoa, Maparsi, Mabanyani, Maajem, watu wa Sini, wa Japan, watu wa Shirazi na wengine wengi.

Afrika ni nchi yetu, nchi ya mbegu mweusi:

Mahabshia, Wasomali, Masai, Waganda, Wanyamwezi, Wahehe, Wasangu, Wasagara, Wazigua, Wachaga, Washambala, Wagogo, Wangoni, na wengine wengi.

Marekani ni bara kubwa, nchi ya mbegu mwekundu. Walakini hatta Wazungu wêngi na watu weusi wamehawa huko, wanakaa.

Australia ni nchi ya visiwa vitupu. Kuna kule pia mbegu mwingine. Nao Wazungu wengi wamepanga huko. Australia inaitwa pia Oseania.

63. AFRIKA.

I

Afrika, ndiyo bara yetu, bara kubwa sana. Pakiwa na barabara, nawe ukenda kwa miguu, mwendo wa saa tanu kwa siku, utakaa miezi mitanu au sita, upasue pwani hatta pwani, tokea Bagamoyo hatta nchi ya Kongo: ndio upana wake. Ukitaka kujua urefu wake, utakaa njiani mwaka mzima, hatta umekwisha pasua tokea Kepu hatta Magrebi, maana tokea kusini hatta kaskazini.

Bahari imezunguka bara yetu, ila upande wa Misri pana Kiungo kama shingo la nchi, palipoungana bara ya Afrika na bara ya Asia: upana wake shingo kama mwendo wa saa arbaini kufu-

NCHI YA AFRIKA.

liza tu kutwa kucha, ndio mwendo wa siku saba. Shingo hilo limepasuliwa njia ya maji pa kupitia markebu: ndiyo kazi kubwa, waliyoifanya Wazungu.

II

Mipaka.

Bahari iliyozunguka Afrika si moja. Ukitoka Kepu kuja zako kwa maji hatta Unguja, ukifuliza hatta ufike Ras-Asir (Ras-Gwadafwi ya Wazungu) ukaabiri bahari ya Hindi, toka kusini paka kaskazini. Tena waelekea mtueo ya jua, hatta ufike Perim: ukaabiri Guba la Aden. Waacha Perim mkono wa shoto, ukipitia pa mlango paitwapo Bab-el-Mandeb. Ukesha pita waingia bahari ya Sham, waelekea kati ya mangaribi na jaha, ufulize beina ya Afrika na Bara-Arabu, hatta ufike Swezi, ndio mji wa Misri. Kutoka Suezi, waingia mto ule uliochimbwa na Wazungu, waenda hatta ufike Por-Saidi, waingia bahari ya Katikati, ndiyo bahari iliyo kaskazini beina ya Afrika na Ulaya. Waelekea matueo ya jua, waabiri Mediterane yote mpaka ufike mwisho wake, penye mlango wa maji, katikati ya Maroko, upande wa Afrika, na mji wa Jibraltar katika bara ya Spenyol, upande wa Ulaya. Ukesha penya, warudi

tena kusini, waambaa bara ya Afrika kwa ṅambo ya hapa, wafuliza tu katika bahari ingine, ndiyo bahari ya Atlantiki, waenda vile safari kubwa sana, hatta ufike Kepu. Kepu ndiyo ncha ya bara ya Afrika, upande wa kusini. Basi safari imekwisha: umezunguka-zunguka kwa njia ya maji, hatta ukarejea kuko huko, kuliko mwanzo wa safari yako.

III

Ṅambo ya bahari ya Hindi, mbali sana lakini, upande wa maawio ya jua, pana masiwa ya Oseania; kwa karibu zaidi pana masiwa ya Sesheli, na ya Ungazija, na ya Moheli, na ya Maoti, na Nosi-Be, na Bukini, na Baribo, na Misri.

Ṅambo ya bahari ya Sham, pana Bara-Arabu; Bara-Arabu ndio sehemu ya Aṣia; kunako na nchi ya Hindi, na nchi ya Ajem, na nchi ya Sini na visiwa vya Yapan.

Ṅambo ya maji ya katikati, ndipo panapo Ulaya: nchi ya pwani ya Mediterane katika Ulaya, ndiyo: Bara ya Turki, ya Ugreki, na Uitalyani, na Ufransa, na Spenyol.

Ńambo ya Bahari Atlantiki, kwa mbali sana. upande wa Matueo ya jua, pana Baja ya Marekani.

IV

Nchi na makabila.

Bara ya Afrika ina nchi nyingi na makabila mengi.

1)

Upande wa kaskazi, pana Misri, na Tripoli, na Magrebi kunako mji wa Alje; pana na Maroko. Nchi hiza zote zimepakana na bahari ya Mediterane kwa upande mmoja, ndio upande wa jaha; kusini zimepakana na uwanja mkubwa, ndiyo Sahara, kusini kwa Sahara kuna bara ya Sudan.

2)

Upande huu wetu, maana upande wa maawio pana bara ya Nubi, na Uhabshia, na bara ya Somali, na bara ya Gala, na bara Swahili, na miji yake Amu, Malindi, Mombasa (Mvita), Tanga, Bagamoyo, Daressalam, Lindi; tena wafika Msumbiji kwa Mrenu, baadaye nchi zote za kusini ni za Mngreza, hatta Natal na nchi ya Wazulu mpaka Kepu.

3)

Upande wa matueo, pana nchi nyingi sana: Nchi ya Damara na Anama, Angola, Kongo, Kamerun, Nigeria ya chini, Nigeria ya juu, Togo, Liberia na Senegambia.

V.

Mito.

Ipo mito mingi: mingine mikubwa sana, kama Nili, na Niger, na Kongo, na Zambezi; mingine iliyo upungufu, kama mito yetu: Pangani, na Wame, na Kingani, na Rufiji, na Rovuma.

VI

Maziwa ya maji.

Yapo na maziwa makubwa ya maji, kama Nyanza, na Tanganyika, na Nyasa, na Chadi. Maziwa mengine upana wao mdogo zaidi, kama Kivu, na Manyara, na Naiwasha na mengine mengi.

VII

Milima

Ipo milima mirefu sana, kuzidi metri alfu tanu, kama Kilimanjaro, na Meru, na Kenya, na Ruwensori. Mengine imezidi metri alfu nne kama Atlasi katika nchi ya Maroko. Milima iliyopata urefu wa metri alfu mbili na tatu mingi sana.

VIII

Nyama.

Nyama-mwitu wako wengi sana. Wakubwa hasa ndizo: tembo, twiga, pofu, kiboko, shikiro, palahala; wengine wakali kama simba, chui, faru, nyati, mamba. Pana na nyama wengine wa namna nyingi: kongoni, kuro, punda-milia, mbala, kulungu, dondoro, swala, paa, mohanga, kakara, fisi, nguruwe, ngiri; Pana Kima, wengine kimo chao kidogo, kama vitumbiri; wengine kimo chao kikubwa, kama manyani; wengine wakubwa zaidi hupata kimo cha bin-Adamu, wapo upande wa Kongo.

Pana na nyoka namna kwa namna, toka chatu hatta nyoka-ukuti.

Ndege wakubwa wako, kama mbuni, mwari, nyamkuta, korongo, furkombe, kirere, pungu, tai,

mumbi, bundi, kipanga, mwewe, na wengine wengi sana wa killa namna.

64. AFRIKA YA MASHARIKIM.

I

Mipaka.

Nchi yetu, ndiyo Afrika ya masharikini, ndio mrima toka Vanga mpaka mto Rovuma, na toka pwani mpaka maziwa Nyasa, na Tanganyika. Mpaka wake kaskazini, ndiyo British-East-Afrika: waenda toka Vanga hatta Kilimanjaro, waamba Kilimanjaro kwa kaskazini, tena waenda sawa sawa, waamba Kavirondo kwa kusini, wapasua Nyanza katikati, wafuliza sawa sawa hatta kufika nchi ya Kongo.

II

Makabila.

Yamo makabila mengi. Waswahili wako pwani. Kwa nyuma yao wako Wadigo, Wabonde, Washambala, Wazigwa, Wagwere, Wadoe, Wazaramo, Wakami, Wakutu, Wangindo, Wamakonde. Nyuma ya makabila hayo wapo Wapare, Wachaga, Warangi, Wasandawi, Wagogo, Wanguru, Wahehe, Wamahenge. Ndani ya mapori wapo Wamasai,

Nyuma kabisa, upande wa maziwa, wapo Wanyamwezi, Wasumbwa, Waruanda, Warundi, Wafipa Wasangu, Wabena na Wangoni.

III

Mito.

Mito mirefu ya kufika pwani, ndiyo Pangani, Wame, Kingani, Rufiji, Rovuma. Mlagarasi mkubwa nao, wapeleka maji yake katika Tanganyika.

IV

Maziwa ya Maji.

Baada ya Nyanza na Kivu, na Tanganyika, na Nyasa, ndiyo maziwa makubwa yaliyo mpakani, upande wa matueo, pana viziwa: Ihema, Urigi, Eyasi au Nyarasa, Manyara, na Rikwa, na vingine vidogo kama Jipe.

V.

Milima.

Kilimanjaro kina ncha zake mbili: Kibo na Kimawenzi; vimepata urefu karibu na metri alfu sita. Meru yapata metri karibu na alfu tanu. Gurui na Lerobi zimezidi metri alfu tatu. Baadaye pana milima mingine iliyozidi metri alfeini katika Pare, na Nguru, na Uruguru, na Ruanda, na Usangu.

VI

Miji.

Miji mikubwa ya pwani: baada ya Dari-salam, ndiyo mji mkubwa zaidi, pana Tanga, Pangani, Bagamoyo, Kilwa na Lindi. Barani pana Korogwe, Wilhelmstal (Rusoto), Moshi na Arusha, upande wa juu. Muanza na Bukoba pwani ya Nyanza. Upande wa matueo, pana Usumbwa, Ujiji, na Songea. Katikati pana: Tabora, Dodoma, Irangi, Iringa, Kilosa, Morogoro, Mahenge.

65. HADISI YA AFRIKA YA KASKAZINI.

Watu wa asili, waliokaa katika bara ya Afrika, hatuna habari nao. Habari tuliyojua ya mambo ya kale ndiyo kama zamani za Ibrahim, Wamisri wakawa watu wakubwa, wenye busara sana na nguvu. Wamisri wakawa na ezi miaka mingi sana; têna wakaingia Wagreki, wakaja Waroma, wakazitwalia nchi zote za Magrebi na Misri.

Zamani za Rabbi etu Yesu Kristu, ndio Waroma waliokuwa wenye nchi. Mitume wakapeleka maaskafu katika bara ya Misri, na bara ya Magrebi; Mtakatifu Matei, mtume, na mtakatifu Marki, mwenjili, wakaja wenyewe. Wakapenya, wakafika inchi ya Nubi, na Uhabshia. Wakati huo Kanisa ikafana sana: pakawa na walimu wa Dini: mt. Sipriani, mt. Atanasi, mt. Augustini, mt. Sirili wa Skanderia. Pakawa na watakatifu wakubwa, kama: mt. Antoni, mt. Makari, mt. Pakomi, mt. Monika; na mashahidi wa Dini, kama: mt. Emîli, mt. Felisi, mt. Teodor, mt. Katarina, mt. Felisite, mt. Perpetua. Basi miaka ilipotimia kama mia tatu baada ya kupaa Rabbi yetu, kurudi kwake uwinguni, palikuwa na maaskafu wengi katika bara ya Afrika kaskazini, jumla yao, kama mia tatu.

Illakini zamani hizo, wakristu wengine wakaase,

wakafanya fitina, wakawapoteza nduguzo wêngi. Hassa mfitini mmoja akaharibu sana Dini, ndiye Ariusi wa Skanderia. Watu wengi wakamfuasa wakaacha Dini ya kweli.

Mwinyezi Mungu akawakasirikia, akawatoa mikononi mwa adui zao. Hatta kama miaka saba mia toka kuzaliwa kwake Yesu Kristu, Waislam wakaingia bara ya Afrika ya kaskazini, wakawatwalia nchi zote, wakawavunja Wakristu, wakawaua wengi. Baadaye Wazungu wakaivunja ezi ya Waislam; hatta leo Wazungu wanatawala nchi zote za Afrika ya kaskazini.

66. HADISI YA BARA SWAHILI.

I

Zamani za kale, watu weusi walikuwa wenye inchi zote. Hatta fitina ilipoingia katika inchi ya Islamu, Arabuni na Ajem, wenye waliopunguka nguvu wakahama, wakaja kukaa katika bara yetu. Walitangulia Maajem, wakapakia katika vyombo vyao, wakaabiri toka Shirazi mpaka kwetu. Wakashukia Kilwa wakajenga boma. Na zamani hizo ndiyo kama miaka alfu, toka kuzaliwa Mwokozi wetu.

II

Washirazi wa Kilwa wakapata nguvu sana; sultani wao akatawala Mafia, na Unguja, na Pemba, na Mrima wote, tokea Msumbiji hatta Malindi. Baadaye, masheki wa Unguja, na Mvita, na Malindi hawakupatana na Sultani wa Kilwa, wakamwambia kwa heri, wakatawala peke yao, wakajifanya masultani, killa sheki katika mji wake.

NCHI YETU
(Tanganyika-Territory).

III

Kama miaka alfu na mia tanu baada ya kuzaliwa Yesu Kristu, wakaja Warenu. Walitoka Ulaya, waliambaa bara ya Afrika upande wa matueo ya jua, wakazunguka Kepu, wakafika Kilwa. Kwanza wakapatana na Sultani wa Kilwa, wakamfanya raya ya mfalme wao. Masultani wa Unguja, na Mvita, na Malindi, wasipokubali, wakashindwa na Warenu. Muda wa miaka selasini, mrima wote, toka Msumbiji hatta Amu, ukawa ukitoa kodi kwa Mrenu. Wenyewe Warenu wakajenga ngome, moja katika kisiwa cha Kilwa, ya pili katika kisiwa cha Mvita. Wakaja na Mapadri warenu, wa shirika la mt. Augustini, na la mt. Dominiki, wakajenga makanisa madogo Unguja, Mvita na Faza. Wakawa wachache; kazi yao kuwasomea Misa Wazungu wao, wasiache pwani. Hatuna habari kama walibatiza watu weusi wengi wakati huo.

Ndipo napo aliposafiri mt. Fransisi Zaveri, kwenda Goa, kuwafundisha Wahindi; akashukia Malindi siku moja tu, akafuliza safari.

IV

Warenu wakatoza kodi zaidi ya miaka miateini. Baadaye Waislam wa mrima wakiona nguvu ya

Warenu imepungua, wakaase, wakaweta Waarabu wa Maskati: ndipo walipokuja Wamaskati. Warenu na Wamaskati wakashindana miaka mingi; hatta mwisho, Warenu wasifae tena, kwa sababu askari zao haba, wakaacha bandari walizoshika kwanza, wakênda zao, wasirudi tena.

Toka hapo, yapata miaka miateini. Wamaskati wakaweka maliwali mijini: sultani alikaa Maskati. Maliwali wasipatane. walitakana vita marra kwa marra. Hasa maliwali ya Amu na Mvita walikuwa na uadui. Sultani wa Maskati akawa na shida sana, maliwali wakimwase killa siku. Hatta mwisho Said-Sayid akatoka Maskati, akaja zake Mvita na Unguja, aone habari kwa macho yake.

Said-Sayid akatawala nchi yote toka Rovuma hatta Kisimayu; akakaa Unguja kidogo, akisafiri marra kwa marra kwenda Maskati. Akafa baharini. (1856).

Alipokufa Said-Sayid, Said-Eweni, ndiye mwanae mkubwa, akarisi usultani wa Maskati, akakaa Maskati; Said-Mejid, mwanae mwingine akarisi usultani wa Unguja, akakaa Unguja, Sultani Said-Mejid akaanza kujenga Daressalam. Baada ya Said-Mejid akatawala nduguye Said-Bargashi (1870—88).

V

Waarabu, tangu kuingia kwao katika nchi, walitengeneza safari, wakienda bara kutaka watumwa. Hupatana na majumbe, majumbe wakiuza watu wao pasipo haki. Waarabu wengine huwashambulia watu katika miji barani, huwatwalia watoto na wânaake kwa nguvu, huwabagua na baba na mama. Wazungu wakapata habari, wala hawakuvumilia uzulumu kama huo. Wakamwambia Said-Bargashi, wakakataza utumwa. Wakimwona sultani hana nguvu ya kuzuia utumwa, wakatia hukumu yao katika nchi za ndani ya bara. Baadaye, wakapatana na Said-Bargashi kwa kugawiana nchi ya pwani, na kufanya hukumu ya haki killa pahali. Wangreza wakatawala Unguja, Mvita (Mombasa), Malindi na Amu. Wadachi wakatawala toka Vanga hatta Mikindani.

VI

Mwarabu mmoja, jina lake Bushiri, akafanya shauri na Waislam wengine, tuwashambulie Wadachi; akashindwa, akakimbia. Hatta alipokamatwa akanyongwa. (1889—90)

Baadaye Mkwawa, ndiye jumbe mkubwa wa Wahehe, akawatakia vita Wadachi, nae akashindwa.

Nyuma ya hayo, makabila mengine wakadanganyiwa na waganga wao, wakafitini; wasifae lakini wakashindwa nao. (1905)

Hapana, wala Mwarabu, wala mtu mweusi aweze kupigana na Mzungu. Wazungu, hasa mapadri, wawatakia mambo mema; mwenye kuwakataa ana wazimu.

67. DINI KATOLIKI KATIKA NCHI YETU.

Katika mwaka 1862 wakaja mapadri wawili wenye kanzu nyeusi, ndio P. Horner na P. Bauri (Etien). Ndio hao waliokuja wa kwanza; yapata zaidi ya miaka hamsini. Mwaka wa sita wakajenga Bagamoyo. Baadaye zikajengwa nyumba nyingine na makanisa katika bara, ndani. Zamani huyo lakini hapakuwa na askafu kwetu.

Nyumao wakaja na mapadri wenye kanzu nyeupe wakafika Unyamwezi na Uganda, wakakaa, wakajenga.

Mwisho wamekuja mapadri wenye kanzu nyeupe na mshipi mwekundu. Wamejenga Daressalam, na katika nchi za Wahehe na Ungoni.

Sasa miji iliyo na mapadri si uchache sana kama kwanza; na maaskafu wako saba.

1) Askafu wa Daressalam. Jimbo lake lina: Uzaramo, Uhehe, Ungoni, Mahenge na Makonde.

2) Askafu wa Bagamoyo. Jimbo lake lina: Ukwere, Udoe, Uzigua, Usagara, Nguru, Uluguru, Kutu, Ugogo, Usandawi.

3) Askafu wa Kilimanjaro. Jimbo lake lina: Tanga, Bondei, Usambara, Pare, Kilimanjaro, Ufiomi na Irangi.

4) Askafu wa Nyanza. Jimbo lake lina: Ruanda, Usuwi na nussu ya Uganda.

5) Askafu wa Unyanyembe. Jimbo lake lina: Unyamwezi, na Turu, na Iraku.

6) Askafu wa Kivu. Jimbo lake lina: Ruanda na Urundi.

7) Askafu wa Tanganyika. Jimbo lake lina: Ufipa, Ukonongo na Usanya.

68. BARUA.

Barua yangu imwendee rafiki yangu Pauli Mzuanda. Salam sana. Na baada ya salamu, nakuambia kama nimeanza kusoma na kuandika kidogo kidogo. Kusali pia nakujua, na kufanya kazi ya killa namna na kucheza machezo mazuri. Walakini mwana-funzi bado, wala si fundi!

Hapa petu pazuri. Hatta watoto wêngi wapo, wênz 'angu wote, na marafiki wangu. Kwanza nilikuwa siwezi sana homa, hatta wengine husema: Iusuf amekwisha! Basi mimi nikaomba sana Mungu Mwinyi mema, nipate afia kidogo, nikanywa dawa, nikapona. Basi sasa napenda kukaa hapa mpaka nisomeshwe barabara.

Nawe rafiki yangu, wasemaje kule Bagamoyo? Umenisahao kweli! Je! Tokea mwaka mzima sikupata habari zako. Basi, mimi sijakusahao, walakini nakuombea Mungu akufurahishe, akujalie nêma zake, akutunze; basi unikumbuke nawe kidogo mbele ya Mungu. Hatta ukipata kalamu, kiraka cha kartasi na kichupa cha wino, basi uniandikie barua nzuri.

Basi mimi nimekwisha.

Wape salam sana, kwanza waalimu wako, ya pili wenz' angu wote.

Barua hii nampa Mabruki mpagazi, akupe mwenyewe. Nampa pia ndoana mbili, shindano moja, na kisu kizuri kikali, zawadi zangu.

Salamu sana! Nimeandika mimi

Yusuf Amakaya

Mandera siku ya 20 ya mwezi Desembri 1892

69. BARUA.

— Barua yangu imwendee rafiki yangu fulani bin fulani.

— Amani juu yako, na rehema ya Mungu, na baraka yake.

— Salamu! mimi nalikuja kwako, siku ya ijuma: nalipewa hati na baba kukuletea. Usubuhi nilipokuja kwako, nisikuone, nikarudi na hati yangu, nikampa mwenyewe. Nimepata habari, punda wako wawili wamekamatwa na simba: sijui ni kweli, ama ni uongo, Mungu ajua.

— Salamu. Nimeandika mimi Abu-Bakari wa Taha al Barawii, mfungo wa kenda, mwezi ishrini. miaka alfu na miateini na tisini.

70. MWENZ' ANGU.

1. Nilikuwa na mwenz' angu,
Rafiki yangu mzuri;
Hatta siku za vita,
Ngoma ikatuita:
«Nye vita! askari!»

2. Risasi we ikavuma,
Ni yako, ama yangu?
Mmoja kalala chini
Kapata kifuani,
Ndiye somo wangu!

3. Mama angu, nasimama;
Mwenyewe ni kunena:
«Nakufa, usikawie,
«Enda upiganie,
«Kwa Mungu kwonana!» P. S.

71. MWINDAJI.

1. Kutumbuza mapori,
Ni kazi yangu nzuri,
Kwani ni mwindaji.
Mwituni kuvizia,

Nyama kuzipigia,
Wangu utendaji.

Kiitikio: { Hali halo, hali halo,
Kwani ni mwindaji.

2. Madege nawapiga
Mahua hatta kanga,
Mti uwapo refu.
Namgundua sikiro,
Kongoni na dondoro,
Nawakoma pofu!

3. Bila hela mfukoni,
Ila maji buyuni
Kipande cha mkate.
Na mbwa wangu karibu,
Sogopi têna tabu,
Nitapenya pote.

4. Mchovu ntalala chini,
Meza yangu majani,
Nipunguze hari.
Kiko têna chawaka,
Nyikani kuzunguka
Kwangu mimi heri!

5. Na jua likitua,
Majiza yakikua,

Napumzika kazi.
Narejea nyumbani,
Na heri na amani,
Mwinyi moyo razi! P. K.

72. UFAJIRI.

1. Ufajiri, ufajiri,
Ukomo wanibashiri.
Tarumbeta kesha pigwa
Ndiyo säa ya kwuawa
Mimi nae mwenzi wangu.

2. Sijasema, sijasema,
Na ucheshi ukakoma.
Jana ni kupanda frasi,
Leo kupigwa risasi,
Kesho lazwa kaburini!

3. Kwa haraka, kwa haraka,
Bahati ikageuka.
Nini afya na uzuri!
Bure huamini umri,
Killa ua lafifia!

4. Nitulie, nitulie,
Kwa Mungu nivumilie.

Japo sitôna jioni
Kwa moyo nende vitani
Nife kufa kwa shujaa. P. K.

73. PAKAWA NA KIBUTI.

1. Pakawa na kibuti — buti,
   Kisicho — o — o — ona bahari.
2. Baada ya juma tatu nne,
   Vyakula vi — vi — vimeishia.
3. Vikesha, zikapigwa kura
   «Aliwe na — na — nani? tusife!»
4. Kanasa mmoja, mdogo wao,
   Msafiri msa — sa — safara kwanza.
5. Kaomba: «Mtakatifu Barba
   «Ni nyama? Mi — mi — miye tafunwe?»
6. Marr' hapo, joshini mwa chombo,
   Zikaja sa — sa — samaki nyingi.
7. Kaachwa, wazitafunie,
   Wazishe sa — sa — samaki zote.
8. Hadisi mukichoka nayo,
   Semeni ni — ni — nirudi nayo! P. S.

74. NLIPITA PA KIMWITU.

1. Nlipita pa kimwitu,
   Pana mwigo kwimba;

Na wimbo wake kiamba:
«Ngo, ngo, ngo, ngo, ngo, ngo!»
Nimesikia kiimba:
«Mvunje shingo, mvunje shingo!»
Nami basi nikaki — ki — ki — ki
Nami nkakimbia.

2. Nlitoka na usiku,
Fisi ni kulia
Mlio wake hasikia:
«Huhu, huhu, huhu»
Maana ni kuzania
«Tamu mguu. tamu mguu»
Nami nikapiga mbi — mbi — mbi
Nikapiga mbio!

3. Nilingia magugu,
Nyenje ndiko kwao;
Nikaumwa masikio
«Zi — zi, zi — zi, zi — zi.»
Je! n' nini usemi huo?
«Mchume ngozi, mchume ngozi.»
Mimi basi nikaku — ku — ku
Mimi nkakupuka!

4. Nlitaka koga huku;
Mna vyura ziwani:
Mama angu! wana ni?

«Kora, kora, kora!»
Hao wanitakiani?
«Mabakora, mabakora!»
Nami juu nikaru — ru — ru.
Nami nikaruka!

75. MWUZA BUYU.

1. Mwuza — buyu yuna nyumba,
Isi nguzo wala mwamba:
Ampangisha mbayuwayu.
Wamwonaye Mwuza — buyu?
Ah! Ah! nimekiri
Mwuza — buyu ni mtu mzuri!

2. Mfuma ndifu kanzuze we!
Moja kartasi nyeupe we!
Kivaa siku ya mvua,
Na siku ya kupakia.
Ah! Ah! nimekiri,
Mfuna difu ni mtu mzuri!

3. Mfuga chawa yuna paka,
Was'o kula panya, haha!
Mmoja hana kucha vino,
Hukwea ngazi kwa mêno,
Ah! Ah! nimekiri
Mfuga chawa ni mtu mzuri!

4. Mtunga lulu jicho moja
Limelekea Unguja,
Moja liko Bagamoyo;
Yana mbisho ndiyo siyo.
Ah! Ah! nimekiri,
Mtunga lulu ni mtu mzuri!

5. Mkama panya yuna mbuzi:
Mbili kweli hula ndizi,
Wa tatu hunywa maziwa,
Kambeba kilima miwa
Ah! Ah! nimekiri,
Mkama panya ni mtu mzuri!

6. Mganga wao nyingi dawa;
Mkitoa kwake mtapewa,
Vita homa, dawa ngapi?
Mganga mgonjwa, dawa ipi?
Ah! Ah! nimekiri,
Mganga wao ni mtu mzuri!

76. MKIWA GEREZANI.

1. Ni mkiwa mbali na mama,
Nafungwa gerezani,
Kulia na kulalama,
Kutwa kucha jizani!

2. Ni mateka bila haki,
Killa huniachia;
Maadui, marafiki
Pia wanichukia.

3. Baba, Mama, hatta ndugu,
Kwao ndiyo kaburi.
Ni Mgeni, mjua uchungu,
Ni Mkiwa sina heri!

4. Sikujaaliwa kamwe,
Sina raha kabisa;
Tafazali nsizaliwe,
Nsijue tâbu sasa.

5. Jiza tupu gerezani,
Na mazito mapingu;
Kutwa kucha vifungoni,
Ngumu mno hali yangu!

6. Ee Mungu wa rehema!
Mja wako msikilie:
Niombayo ndiyo nêma
Mbinguni nifikie!

P. S.

77. MSOMO WA KILATINI.

Maneno ya kilatini ndiyo maneno ya Warumi, watu wa zamani. Hatta Mitume wa Bwana wetu Yesu-Kristu walipokuja Roma, wakatumia maneno yale ya kilatini wafundishe watu, wasali Mungu. Basi, ndiyo sababu maneno yale yatumika Kanisani mpaka leo.

Soma maneno ya kilatini sawasawa kana kusoma maneno ya kiswahili, na tafauti hizi tu:

1° **Æ** na **Œ** yatolewa kana **E.** Beatæ = Beate.

2° **C** yatolewa marra moja kama **s,** marra ingine kama **k;** Basi, **C** ikitangulia **e, i,** soma **Ce, ci,** = **Se, si; C** ikitangulia **a, o, u,** soma **ca, co, cu,** = **ka, ko, ku!** Cœlum, cibus, cantus, coram, cuncti. Soma selum, sibus, kantus, koram, kunkti.

3° **Q** yatolewa kama **K:** Qua, quae, qui, quo, quod; soma: **k**wa, **k**we, **k**wi, **k**wo, **k**wod.

4° **X** yatolewa kana **Gz** au **Ks.** Exitu, soma: Egzitu; dixi, soma: diksi.

5° **T** ikitangulia **a, e, i, o, u,** katikati ya neno, yatolewa kana **ts.** Gratias, totius, soma: gra**ts**ias, totsius.

6° **Y** yatolewa vilevile kana **I**; Martyr, Moyses, soma: Martir, Moises.

7° **J** yatolewa vilevile kama **Y;** Jesus, soma: Yesus.

† In nomine Patris, et Filii et Spiritus Sancti. Amen.

ORATIO DOMINICA

Pater noster qui es in coelis, sanctificetur nomen tuum, adveniat regnum tuum, fiat voluntas tua sicut in coelo et in terra.

Panem nostrum quotidianum da nobis hodie, et dimitte nobis debita nostra sicut et nos dimittimus debitoribus nostris, et ne nos inducas in tentationem, sed libera nos a malo. Amen.

SALUTATIO ANGELICA

Ave, Maria, gratia plena, Dominus tecum, benedicta tu in mulieribus et benedictus fructus ventris tui Jesus.

Sancta Maria, Mater Dei, ora pro nobis peccatoribus, nunc et in horâ mortis nostrae. Amen.

Gloria Patri et Filio, et Spiritui sancto : Sicut erat in principio, et nunc et semper, et in saecula saeculorum. Amen.

SYMBOLUM APOSTOLORUM

Credo in Deum, Patrem Omnipotentem, Creatorem coeli et terrae; et in Jesum Christum,

Filium ejus unicum, Dominum nostrum; qui conceptus est de Spiritu Sancto, natus ex Maria Virgine; passus sub Pontio Pilato, crucifixus, mortuus, et sepultus; descendit ad inferos, tertia die resurrexit a mortuis; ascendit ad coelos, sedet ad dexteram Dei Patris Omnipotentis; inde venturus est judicare vivos et mortuos.

Credo in Spiritum Sanctum, Sanctam Ecclesiam Catholicam, Sanctorum Communionem, Remissionem peccatorum, carnis Resurrectionem, Vitam aeternam. Amen.

De profundis clamavi ad te, Domine : * Domine, exaudi vocem meam.

Fiant aures tuae intendentes * in vocem deprecationis meae.

Si iniquitates observaveris, Domine, * Domine, quis sustinebit?

Quia apud te propitiatio est, * et propter legem tuam sustinui te, Domine.

Sustinuit anima mea in verbo ejus; * speravit anima mea in Domino.

A custodia matutina usque ad noctem, * speret Israel in Domino.

Quia apud Dominum misericordia, * et copiosa apud eum redemptio.

Et ipse redimet Israel * ex omnibus iniquitatibus ejus.

℣ Requiem aeternam dona eis, Domine.

℟ Et lux perpetua luceat eis.

Magnificat * anima mea Dominum.

Et exsultavit spiritus meus * in Deo salutari meo.

Quia respexit humilitatem ancillae suae, * ecce enim ex hoc beatam me dicent omnes generationes.

Quia fecit mihi magna qui potens est; * et sanctum nomen ejus.

Et misericordia ejus a progenie in progenies * timentibus eum.

Fecit potentiam in brachio suo; * dispersit superbos mente cordis sui.

Deposuit potentes de sede, * et exaltavit humiles.

Esurientes implevit bonis, * et divites dimisit inanes.

Suscepit Israel puerum suum, * recordatus misericordiae suae.

Sicut locutus est ad patres nostros, * Abraham et semini ejus in saecula.

3 5282 00435 0701

3 5282 00435 0701